# SIMULIZI ZA AZIMIO LA ARUSHA

KAVAZI LA MWALIMU NYERERE
NYERERE RESOURCE CENTRE

# SIMULIZI ZA AZIMIO LA ARUSHA

Kimetayarishwa na kuhaririwa na

**Bashiru Ally**

**Issa Shivji**

Chapisho Maalumu, 2017

Kimetayarishwa na kuhaririwa na Bashiru Ally na Issa Shivji
Kimechapishwa na Kavazi la Mwalimu Nyerere
Toleo la Kwanza 2017

© Kavazi la Mwalimu Nyerere

ISBN: 978-9976-9903-5-5

Kitabu hiki kimechapishwa kwa hisani ya Rosa Luxembourg Stiftung (RLS) inayofadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Ujerumani

Kimechapwa na Inter Press of Tanzania Ltd, Dar es Salaam.

# Yaliyomo

**Dibaji**........................................................................................ 2

*Issa Shivji*

**Sura ya Kwanza**

Uchambuzi Mfupi wa Azimio la Arusha...................................... 4

*Issa Shivji*

**Sura ya Pili**

Azimio la Arusha........................................................................ 16

*Tanganyika African National Union*

**Sura ya Tatu**

Azimio ni Matumaini ya Waliowengi.......................................... 36

*Julius Nyerere*

**Sura ya Nne**

Kila Zama na Kitabu Chake......................................................... 44

*Ali Hassan Mwinyi*

**Sura ya Tano**

Miongozo Miwili ya Chama na Tabaka Lililopindua Ujamaa...... 60

*Issa Shivji*

# Dibaji

*Simulizi za Azimio la Arusha* ni chapisho maalum la Kavazi la Mwalimu Nyerere liloandaliwa kwa ajili ya maadhimisho ya miaka hamsini ya Azimio. Kavazi limenuia kuufanya mwaka wa 2017 kuwa mwaka wa Azimio la Arusha. Tunaanza na simulizi za Azimio la Arusha, tarehe 22 Februari na baada ya hapo tutaendelea, hadi mwishoni mwa mwaka, kuandaa matukio mbalimbali yanayolenga kusimulia, kujadili, kutafakari, kudadisi na kulichambua Azimio pamoja na kuainisha mafunzo yanayotokana na falsafa, itikadi pamoja na utekelezaji wake.

Ni kawaida siku hizi kuwasikia baadhi ya wasomi, wanasiasa na wanahabari wakisema kwamba nchi yetu imekosa dira. Mara nyingi wanasema hivyo bila kuangalia kwa undani kuhusu dhana na maana ya dira. Sura ya Kwanza inachambua, kwa muhtasari, mpangilio wa Azimio na misingi yake kwa mtazamo wa kifalsafa na kiitikadi. Matumaini yetu ni kwamba uchambuzi huu utaongeza kiwango cha uelewa wa wasomaji kuhusu dhana na maana ya dira.

Sura ya Pili ni Azimio lenyewe. Siku hizi ni nadra kupata kijitabu cha Azimio. Kwa hiyo, tumeona ni vyema tukachapisha tena waraka huu muhimu wa kihistoria.

Sura ya Tatu ni sehemu ya hotuba ya Mwalimu Nyerere aliyoitoa katika semina ya wakuu wa serikali, mashirika ya umma na wafanyabiashara mwaka 1989. Katika kipindi cha kwanza cha uongozi wa awamu ya pili, chini ya Mzee Mwinyi, vuguvugu la kupinga Azimio lilikuwa limeshaanza. Hoja ilikuwa kwamba Azimio limepitwa na wakati na hatuwezi kuachwa nyuma wakati dunia nzima imekubali kwamba Ujamaa umeshindwa na ubepari hauepukiki. Wengi wa wasomi wetu walikubaliana na hoja hizo. Aidha, tulikuwa tumeanza kulegeza masharti ya biashara, na kukubali masharti ya

taasisi za fedha za kimataifa pamoja na wafadhili. Mwalimu alitoa hotuba hiyo katika mazingira hayo na alitumia fursa hiyo kuwaonya viongozi na watawala wasifanye kosa la kuachana na Azimio kwa sababu ndilo hasa lililotoa matumaini kwa wanyonge. Mwalimu aliamini kwamba Wananchi wakikosa matumaini, mfumo mzima wa serikali na utawala utakosa uhalali na kutokana na hali hiyo hakutakuwa na sababu ya Watanzania kuendelea kuwa watulivu. Watanzania watatuliaje kama hawana matumaini ya kesho? Mwalimu alihoji.

Hata hivyo, watawala hawakumsikiliza. Katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya Chama cha CCM, uliofanyika huko Zanzibar mwaka 1991 chini ya Mzee Mwinyi, viongozi wa juu wa chama walifanya maamuzi ya kulegeza masharti ya uongozi, yaani, kuruhusu viongozi wa chama na serikali kujilimbikizia mali. Sura ya Nne ni hotuba ya Mzee Mwinyi inayoelezea na kutetea maamuzi ya Zanzibar. Katika hotuba hiyo, Mzee Mwinyi anasisitiza kwamba maamuzi yale yalikuwa ni tafsiri mpya ya Azimio ili nchi iweze kuendana na wakati!

Sura ya Tano na ya mwisho ni uchambuzi wa Miongozo miwili ya Chama, Mwongozo wa 1971, na Mwongozo wa 1981. Mwelekeo wa uchambuzi huo ni kuonyesha kwamba tabaka la warasimu lililojengeka chini ya mwavuli wa Azimio ndilo lililoanza vuguvugu la kuachana nalo ili tabaka hilo lipate nafasi ya kutanuka na kutamalaki.

Ni matumaini yetu kwamba maandishi haya yatavisaidia vizazi vya leo kuelewa kwa undani historia ya Azimio la Arusha na kutoa mchango wao katika kukomboa nchi na bara letu.

Issa Shivji
Mkurugenzi, Kavazi la Mwalimu Nyerere
Februari 2017.

# Sura ya Kwanza

# Uchambuzi mfupi wa Azimio la Arusha

Issa Shivji*

## Kupaa na Kuanguka kwa Azimio

Mnamo tarehe 5 Februari 2017, Azimio la Arusha lilitimiza miaka hamsini, au nusu karne, tangu kuzaliwa kwake. Bila shaka, Azimio lilikuwa waraka mojawapo wa kimapinduzi ulioandaliwa na kutekelezwa barani Afrika. Kwa wakati wake, na katika mazingira ya mapambano ya ukombozi nyakati zile, Azimio liliwafarijisha na kuwatumainisha Waafrika kote duniani. Kama uhuru wa Ghana ulirejesha heshima ya Mwafrika, kama alivyosema mmajumui maarufu, C.L.R. James,[1] basi Azimio lilikuwa ni matumaini ya mnyonge kujikomboa kutokana na makucha ya unyonyaji, umaskini na udhalilishwaji. Kauli mbiu ifuatayo ya Azimio ilipokelewa kwa shangwe, ikawa wimbo wa kitabaka wa wavujasho:

> Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, na tumepuuzwa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka mapinduzi; mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena, tusinyonywe tena na wala tusipuuzwe tena.[2]

## Ujio wa Azimio

Azimio halikukuja kama mwujiza au kutokana na fikra za mtu mmoja tu. Ni kweli kwamba Mwalimu Julius Nyerere alikuwa na fikra za kijamaa na chama chake chenyewe, TANU (Tanganyika African National Union) kilitaja ujamaa kama mojawapo ya malengo yake. Hata hivyo, Ujamaa kama visheni na itikadi ulikuwa haujakomaa. Azimio ni matokeo ya mapambano

---

*Mkurugenzi, Kavazi la Mwalimu Nyerere, Tume ya Sayansi na Teknolojia, Dar es Salaam.

ya kisiasa na kifikra yaliyopamba moto mara baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1961.

Walioshiriki katika mapambano ya uhuru, wakiwa wanachama na viongozi wa TANU pamoja na vyama vya wafanyakazi na vyama vya ushirika, walikuwa na maslahi mbalimbali na tafsiri tofauti ya uhuru kutokana na hali yao halisi. Jambo ambalo liliwaunganisha na kuwashawishi wajiunge na vuguvugu la kudai uhuru ni moja – hawakutaka kuendelea kutawaliwa na kubanwa katika kutafuta heshima kama binadamu na kuishi kama wanadamu huru. Lakini kila mtu na kila kikundi kilikuwa na mtazamo wake kuhusu uhuru na hata matarajio yake baada ya uhuru.

Mara baada ya uhuru, mitazamo na maslahi ya vikundi mbalimbali yakaanza kugongana. Walioshiriki katika mapambano ya uhuru, hasa makada wa kati na chini, wakajikuta wanakosa vyeo mbalimbali vya kisiasa na utumishi serikalini kutokana na kutokuwa na sifa za kielimu. Wale ambao walipata nafasi hizo kutokana na sifa zao za kielimu hawakushiriki kikamilifu katika mapambano ya uhuru. Kwa hiyo, walihisi wamekosa matunda ya uhuru, na wasioshiriki ndio waliofaidika.[3]

Wafanyakazi walitarajia kupata nafuu katika hali yao ya kazi. Kwa kiasi fulani maslahi yao yaliboreshwa lakini bado waliachwa mbali na watumishi wengine kama wahindi na wazungu. Kwa hiyo, wakaona ule ubaguzi wa rangi wa kikoloni walioupinga unaendelea. Viongozi wa vyama vya wafanyakazi pia wakaona hawapewi nafuu zaidi kuliko watu weupe na kwa hivyo walikuwa mstari wa mbele kupigania Afrikanaizesheni, kwa maana ya upendeleo kwa wazawa. Kwa jumla, mtazamo wao wa kibwanyenye uliwaaminisha kwamba wao ndio wanaostahili kuchukua nafasi za wakoloni na vibaraka wao wahindi.

Mwalimu na wenzake wachache walikuwa na mtazamo tofauti. Mtazamo wao ulikuwa ni kubuni na kuongoza utekelezaji wa mradi wa kujenga taifa kwa kusimika na kuimarisha misingi ya umoja na uraia na kubomoa misingi ya ubaguzi wa kikabila, rangi au dini iliyosimikwa na wakoloni. Pamoja na

migongano hii ya kimtazamo, ambayo iliendelea, jambo baya zaidi ni kwamba walioingia madarakani walianza kwa kasi kubwa kutumia vyeo vyao vya kisiasa kujilimbikizia mali, hususan nyumba za kuishi na za kukodisha, na walianza kuishi maisha ya anasa. Kwa hiyo, matabaka yakaanza kujengeka miongoni mwa Waafrika. Mwalimu aliona jambo hili kama hatari kwa uhalali wa serikali yake na halikuendana na mtazamo wake kuhusu maana na matarajio ya uhuru.

Misiguano hiyo miongoni mwa makundi haya ya kibwanyenye ilijitokeza waziwazi katika mgomo wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambao walikuwa wanapinga mpango wa kujitolea katika Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Mnamo mwezi Oktoba 1966, wanafunzi waliandamana huku wakisindikizwa na polisi kwenda viwanja vya Ikulu. Katika risala yao waliyoisoma mbele ya Mwalimu na baraza lake la mawaziri, wanafunzi, pamoja na mambo mengine, walisema bila kutafuna maneno:

> Ikiwa kama viongozi hamtabadili msimamo wenu, sisi hatutakubali kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Mnaweza mkapeleka miili yetu jeshini, lakini roho zetu zitabaki nje ya huo mpango. Na vita baina ya wanasiasa na wasomi itaendelea daima.[4]

Mwalimu akakasirika, tena sana.

> Sitampeleka mtu yeyote jeshini ambaye roho yake haimo humo. … … Jeshi sio gereza. Amueni. Mie sitatumia, sitatumia, sitatumia hela za wananchi kumsomesha yeyote ambaye anasema Jeshi la Kujenga Taifa ni gereza.[5]

Alipomaliza, Mwalimu akawaambia vijana: "Nendeni nyumbani". Walipotoka nje ya viwanja vya Ikulu, vijana wakawakuta polisi wanawasubiri. Wakapakiwa katika mabasi kwenda Chuoni kukusanya mizigo yao na kupelekwa hadi vijijini kwao wakisindikizwa na polisi. Wanafunzi takriban 400 wakafukuzwa na Chuo kikafungwa kwa miezi kama tisa kabla wanafunzi kurudishwa.

Huu ulikuwa ni mwanzo wa kubadili sera, siasa, mwelekeo na mtazamo wa serikali ya Mwalimu. Miezi michache baada ya tukio la wanafunzi, Mwalimu alifanya ziara ya mikoa takriban minane akihutubia wananchi mijini na vijijini kuhusu hali halisi ya nchi na mipango na mitazamo mipya ya serikali yake. Katika ziara hizo alitoa hotuba nzito takriban 12. Hatimaye, ziara zake ziliishia Arusha ambako, kwa mara ya kwanza katika hotuba yake kwa wakuu wa mikoa tarehe 23 Januari 1967, alitoa hadharani alichokuwa anawazia. Katika mkutano wake uliofuata kati ya tarehe 26 na 29 Januari 1967, Halmashaurti ya Chama cha TANU ilijadili na hatimaye kupitisha Azimio la Arusha.

Katika hotuba yake ya ufunguzi wa kikao cha Halmashauri Kuu, Mwalimu alizungumza kwa saa tatu akieleza maana ya Ujamaa, akichambua sifa za uchumi tegemezi na umuhimu wa kujitegemea, na akibainisha jinsi mabwanyenye wa nchi za Magharibi wanavyonyonya jasho la wazalishaji wa Afrika pamoja na Tanzania. Ni vyema nimnukuu Mwalimu mwenyewe hasa namna alivyoeleza kwa ufasaha maana ya unyonyaji na nafasi ya nchi maskini chini ya himaya ya kibeberu ulimwenguni:

> Kuna mfano mmoja ambao nadhani utasaidia sana kueleza jambo la unyonyaji. Wazee wa Uzanaki hunywa pombe kutoka katika chungu kimoja kwa kutumia mirija. Kila mzee huwa na mrija wake. Wazee hao kutwa wananyonya pombe chini ya kivuli. Huko ndani kuna mitungi ya pombe. Kuna watu kazi yao ni kuchemsha maji, maana pombe hiyo hutiwa maji ya moto. Kuna watu kazi yao ni kuona kuwa pombe haipungui katika chungu. Wengine wanashughulika na uonjaji ili kuwapatia wazee pombe nzuri. Wazee wanakaa na kufyonza tu. Kuna mwiko kuwa huwezi kushika mrija wa mtu mwingine; labda tu kusaidia kuondoa machicha ndani ya mrija.
>
> Sisi tunajitawala kweli? Hapa kwetu kuna mirija tele. Mirija ya Germany, Marekani, Uingereza, na kadhalika.

> Sisi hatuna kimrija hata kimoja kinachokwenda Uingereza au mahali pengine. Tuliwaahidi kama mirija yao itaendelea kuwepo baada ya Uhuru. Amani itakuwepo ili wasiwe na wasiwasi au mashaka. Wananchi wa Algeria iliwabidi kupigana maana mirija ilikuwa mikubwa mno kiasi ambacho waliamua kuikata mirija hiyo moja kwa moja. Takajitawala na tukawa mwanachama wa Umoja wa Mataifa. Tunaanza kusema sisi ni kama waandazi. Sisi ni wa kuangalia kuwa chungu kina pombe na mitungi mingine ina pombe. Wao wanakuja kukagua na wengine wanakuja kumwona President na kumwuliza kama mambo ni sawa sawa. Nawaambia mambo ni safi. Wanauliza, "can we invest more?" Nawajibu "yes". Wanauliza tulete mirija zaidi? Nami nawajibu leteni. Wanauliza, "what about NUTA…". Nawajibu, "don't worry about NUTA …". Yaani wanauliza vipi NUTA, nami nawajibu wasiwe na wasiwasi juu ya NUTA. Tunawapa uhakikisho wasiwe na wasiwasi juu ya mirija yao.[6]

Kwa lugha ya kitabaka, anachosema Mwalimu ni kwamba vibwanyenye wetu ni kama wale wanaochemsha pombe na kuhakikisha kuwa mabwanyenye wa nchi za Magharibi wanaendelea kunyonya pombe kupitia mirija, au mitaji, yao. Jukumu la watawala wetu ni kulinda mitaji yao na kusimamia utulivu ili mirija yao isiwe na misukosuko.

Wasomaji, hususan vijana, wajiulize: Hali ya nchi yetu leo ni tofauti sana na ile Mwalimu aliyohadithia mwaka 1967?
Sasa tuangalie jinsi Azimio lilivyonuia kushughulikia mirija ya nje na walinzi wake wa ndani.

## Undani wa Azimio

Ili kurahisisha uchambuzi wangu wa Azimio, nitatumia dhana ya uhusiano baina ya falsafa, itikadi na sera. Kwa muhtasari, niseme kwamba falsafa

huzaa itikadi; itikadi huzaa programu na sera za utekelezaji. Na kwa jumla haya yote matatu ndio kiini au msingi wa siasa-tawala.

## Viini vya Azimio

### *A. Misingi Mitatu ya Kifalsafa*

Uchambuzi unaonyesha kwamba hoja za Azimio la Arusha zimejengwa juu ya misingi mitatu ya kifalsafa ambayo ndiyo sifa maalum zinazoainisha waraka huo. Misingi hiyo ni:

(a) Usawa;
(b) Uhuru; na
(c) Umajumui ("collectivism")

Usawa wa binadamu ilikuwa dhana kuu na imani thabiti ya Mwalimu mwenyewe aliyoisimamia kwa dhati na uhodari katika kipindi chote cha utawala wake. Uhuru wa binadamu ni uhuru wa mtu mmoja mmoja na jamii au nchi kwa jumla. Na dhana ya umajumui ("collectivism") ni kinyume na dhana ya ubinafsi ("individualism") ambayo ni msingi wa jamii ya kibwanyenye na uchumi wa kibepari. Pamoja na mtazamo huu wa kifalsafa, hii haina maana kwamba katika hali halisi ya kisiasa, haukuwepo uvunjifu wa misingi au mtazamo huu. Lakini hapa sio mahali pake pa kuzungumzia. Uchambuzi huu umejikita kwenye nadharia, sio utendaji.

### *B. Nguzo Nne za Kiitikadi*

Nguzo nne za itikadi zinazotokana na misingi ya kifalsafa ya Azimio ni:

(d) Dira ya kijamaa;
(e) Mfumo jumuishi wa uzalishaji;
(f) Mfumo wa utawala wa kidemokrasia; na
(g) Wajenzi wa ujamaa kuwa ni wakulima na wafanayakazi.

Dira au visheni ya Azimio ni wazi kabisa, nayo ni kujenga jamii na nchi ya kijamaa inayoheshimu na kulinda misingi ya usawa wa binadamu wote; isiyo na ubaguzi wa aina yoyote na isiyo na unyonyaji. Yaani, nchi ya kijamaa haina matabaka ya wanyonyaji na wanyonywaji, au kwa lugha nyepesi, wavunajasho na wavujajasho. Ndio maana, nguzo kuu za uzalishaji hazina budi zimilikiwe na wakulima na wafanyakazi "wenyewe kwa kutumia vyombo

vyao, Serikali yao na Vyama vyao vya Ushirika."[7] Njia zilizotajwa na Azimio ni, "ardhi, misitu, madini, maji, mafuta na nguvu za umeme; njia za habari, njia za usafirishaji; mabenki na bima; biashara na nchi za kigeni na biashara za jumla; viwanda vya chuma, mashini, silaha, magari, simenti, mbolea, nguo, na kiwanda chochote kikubwa ambacho kinategemewa na sehemu kubwa ya watu katika kupata riziki zao au kinachotegemewa na viwanda vingine; mashamba makubwa na hasa yale yanayotoa mazao ya lazima katika viwanda vikubwa."[8]

Aidha, Azimio linasisitiza kwamba haitoshi Serikali kumiliki njia za uzalishaji kama Serikali yenyewe, na Chama kinachoongoza Serikali hiyo, sio cha wafanyakazi na wakulima. Kwa maana hiyo Serikali na Chama chenyewe lazima vyote viwe vya kidemokrasia.

Kwa mantiki hiyo, katika nchi iliyonuia kujenga Ujamaa, wakulima na wafanyakazi ni wajenzi, walinzi na vilevile ni wanufaika wa mfumo wa kijamaa. Kwa mantiki hiyo, viongozi wa Serikali na Chama pia lazima wawe wakulima na wafanyakazi. Huwezi kuhubiri ujamaa wakati wewe mwenyewe sio mjamaa na huwezi kuongoza wakulima na wafanyakazi wakati wewe ni bepari au kabaila. Hoja hizi ndizo chanzo cha yale masharti ya uongozi na ndizo kiini hasa cha kutangazwa kwa Azimio lenyewe. Viongozi wa Chama na Serikali walizuiwa kuwa na hisa au kuwa wakurugenzi katika makampuni ya kibepari au ya kikabaila; kuwa na mishahara miwili au zaidi; na kuwa na nyumba za kupangisha.

Masharti ya uongozi kwa mujibu wa Azimio la Arusha yana chanzo na madhumuni tofauti kabisa na maadili au mgongano wa maslahi ya viongozi ambayo ni masuala yanazungumzwa zaidi siku hizi. Hoja za Azimio kuhusu masharti ya viongozi zina mizizi yake katika mfumo wa kijamaa. Hoja za maadili na mgongano wa maslahi hazipingani hata kidogo na mfumo wa kibepari. Ndio maana nyakati za Azimio mfanyabisahara au mwenye nyumba ya kupangisha asingeweza kuwa mwanachama wa TANU au kiongozi wa serikali au mbunge kama ilivyo siku hizi.

Utaifishaji wa njia kuu za uchumi haukupata upinzani mkubwa kutoka ndani isipokuwa tu makampuni ya nje na hasa mabenki. Lakini masharti ya uongozi yalipingwa na vibwanyenye wa ndani, hususun viongozi wa Chama na Serikali, kwa kuwa walishaanza kuonja matunda ya ubepari. Wengi wao walikuwa na nyumba za kupangisha na wengine walishachukuwa mikopo ya kujenga nyumba za kupangisha.

Mnamo mwezi wa Aprili, 1967 wabunge walipewa nafasi ya kumuuliza Mwalimu maswali kuhusu Azimio. Jambo la kushangaza (au labda sio la kushangaza sana) ni kwamba hapakuwa na swali hata moja lililohusu Ujamaa na Kujitegemea, bali karibu maswali yote yalikuwa juu ya masharti ya uongozi. Miongoni mwa maswali yaliyoulizwa lipo swali ambalo liliingiza mambo ya ubaguzi ambayo Mwalimu alikuwa akiyachukia sana. Mbunge mmoja aliuliza:

> Kama mtu haruhusiwi kujenga na kupangisha nyumba; je, hii si kuzuia Waafrika kujenga majumba Dar es Salaam na katika miji mingine na kuwaachia nafasi hii wahindi na wageni? Hili ni jambo la Busara?[9]

Mwalimu alitambua kwamba swali hilo liliulizwa kihila kwani muulizaji alijaribu kutumia ukabila au rangi kuhalalisha unyonyaji. “Unyoyaji hauna rangi”, Mwalimu alikataa katakata.

> Anayenyonywa hajali kama mwenye mrija au mrija wenyewe ni mweusi, mweupe au manjano. Anachotaka ni kukata mirija, na hali yake haitakuwa bora zaidi kwa kuambiwa kuwa mirija ya kwanza ilikuwa myeupe na manjano lakini hii mipya ni myeusi na maji ya kunde. Mrija ni mrija tu, na halali yake ni kukatwa.[10]

Mwalimu alisisitiza kwamba Azimio, bila kujali rangi au kabila la mtu, linamzuia kiongozi yeyote kuwa bepari lakini halimzuii Mtanzania yeyote, wa rangi yoyote, kuwa bepari au kabaila ilimradi ajue kwamba “kwa kufanya hivyo atakuwa kajinyima mwenyewe kuwa kiongozi wa Chama cha Kijamaa

au kushika kazi ya madaraka katika Serikali ambayo shabaha zake ni za kijamaa."[11]

Mwalimu alishinda kwa nguvu ya hoja lakini suala la kimfumo, ambalo hatimaye lilikuwa la kitabaka, halikuyeyuka. Likaendelea kuwakera viongozi na hata wananchi. Waasia, waliowekeza katika sekta za viwanda na biashara na ambao walikumbwa na dharuba ya utaifishaji, walibadili mkondo wa uwekezaji kwa kuelekeza mitaji yao katika sekta ya nyumba. Viongozi na watumishi wa Serikali wakaanza kulalamika kwamba Wahindi waliendelea kufaidika wakati wao wakizuiwa kujilimbikizia mali. Hatimaye, mnamo mwaka 1971, nyumba za kukodisha zilitaifishwa. Sababu muhimu ilikuwa ya kisiasa zaidi kuliko ya kiuchumi. Ili aweze kutunza na kukuza utii miongoni mwa viongozi wake, na kwa kiasi fulani kurekebisha hali ya kihistoria tulioirithi kutoka kwa wakoloni ambayo ilijenga matabaka kwa msingi wa rangi, ilimbidi Mwalimu kuchukua hatua za maksudi za kusawazisha hali ya utengano na ubaguzi kwa msingi wa rangi. Hatua mojawapo aliyoichukua ilikuwa kutaifisha nyumba. (Hatua nyingine ilikuwa kutaifisha shule za taasisi na jumuiya za dini.)

## Mashina Manne ya Maendeleo

Kwa mujibu wa Azimio, mambo manne ni muhimu kuleta maendeleo. Hayo ni:

(h) Ardhi;
(i) Watu;
(j) Siasa safi; na
(k) Uongozi bora.

Azimio lilidai kuwa tunayo ardhi ya kutosha isipokuwa wakulima wanakosa juhudi na maarifa ya kuzalisha kwa tija. Aidha, Azimio lilisisitiza kwamba kuna haja ya kulima chakula ili taifa liweze kujitosheleza kwa chakula. Hakuna utegemezi mbaya kuliko kuwategemea wengine kwa mahitaji yako ya chakula. Watu, hususan wazalishaji, washawishiwe kufanya kazi kwa juhudi na maarifa na kila mtu afanye kazi halali. Siasa safi ni siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na uongozi bora ni uongozi unaoongoza kwa mfano sio kwa

amri au unyapara. Aidha, viongozi walipitishwa katika tanuri ya mafunzo ya itikadi na mtazamo wa kijamaa.

Hata hivyo, Mwalimu alipinga wazo la kukigeuza Chama kuwa cha makada wateule ("vanguard party") wenye ufahamu wa hali ya juu wa nadharia na siasa ya ujamaa na waliojitolea maisha yao kujenga ujamaa bila kujali maslahi yao. Pamoja na msimamo huo, Mwalimu alitambua haja na umuhimu wa kuwa na mafunzo ya uongozi ambayo yalikuwa yanatolewa na Chuo cha Chama cha Kivokoni.

## Sera za Utekelezaji

Baada ya kuweka misingi ya itikadi na kwa kiasi fulani programu ya maendeleo ndani yaAzimio la Arusha, Chama kilipitisha sera mbali mbali – kwa mfano, elimu ya kujitegemea, ujamaa vijijini n.k. – ili kutekeleza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Na sera hizi na zingine zilikuwa zinarekebishwa mara kwa mara kutokana na hali halisi bila kuathiri misingi ya itikadi na siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

## Hatma ya Azimio: Mitazamo Miwili

Azimio la Arusha halikuwa msahafu mtakatifu. Lilikuwa ni waraka wa kisiasa uliotokana na hali halisi ya mapambano ya kijamii. Mipaka ya upeo wake ilichorwa na mazingira ya kihistoria kwa upande mmoja, na hali halisi ya ukuaji wa mapambano ya kitabaka, kwa upande mwingine. Sio nia yangu kuzungumzia hili. Nia yangu ni kuonyesha misingi mikuu ya mtazamo wa Ujamaa wakati huo kwa kufanya uchambuzi wa waraka wenyewe. Matumaini yangu ni kwamba tutaendelea kulitafakari Azimio la Arusha katika muktadha na nafasi yake kwenye historia yetu pamoja na kujifunza masuala yanayotokana na kupaa na kuanguka kwake.

***

Hatma ya Azimio la Arusha – mafanikio na upungufu wake – yanaweza kuzungumziwa kwa mitazamo miwili mikuu. Mtazamo mmoja, ambao kwa jumla, tunaweza kuuita mtazamo wa kibwanyenye, ni kwamba Azimio

lilikuwa tu ndoto na imani ya mtu mmoja mwenye kipaji kupita kiasi. Katika hali halisi, halikuwa na uwezekano wa kufanikiwa. Utekelezaji wake ulikuwa hafifu na ulisheheni makosa mengi ya kiufundi. Hatimaye, binadamu ni mbinafsi na huwezi kuleta maendeleo bila ya kumpa uhuru wa kufanya anavyotumwa na nafsi na maslahi yake. Azimio lilijaribu kufanya kinyume na hulka ya mwanadamu. Kwa hiyo, kushindwa katika malengo na utekelezaji wake kusingeepukika.

Kwa upande mwingine, kuna mtazamo wa kisoshalisti ambao unadai kwamba binadamu huishi katika jamii na sifa yake kuu ni kwamba yeye ni mmajumui ("social being") na sio mbinafsi. Maendeleo pia ni dhana inayobishaniwa kwa msingi kwamba maendeleo yanayozungumziwa yanaweza kuwa ya waliowengi au wachache. Kwa msimamo huo, Ujamaa ulikuwa na upungufu lakini ulipiga hatua katika kuamsha ari ya wanyonge na nia yao ya kujenga jamii isiyo na unyonyaji, dhuluma na udhalilishaji unaotokana na umaskini na kutawaliwa, kisaisa na kiuchumi. Katika sura ya tano, yamechapishwa makala yangu niliyoandika mwaka 2009. Makala haya yanajaribu kuonyesha, kwa mtazamo wa kitabaka, namna Azimio lilivyopinduliwa katika mapambano ya kitabaka.

Sio nia yangu kutatua mabishano baina ya mitazamo hii miwili ya kifalsafa. Mitazamo hii imedumu kwa karne nyingi tangu ujio wa mfumo wa kibepari na itaendelea. Jibu lake sahihi litapatikana tu kutokana na mwendelezo wa historia yenyewe ya mwanadamu. Safari ya binadamu ya kupata usawa, haki na ustaarabu ni ya karne nyingi. Azimio lilikuwa ni tone tu la mchango wa kifikra na kiitikadi katika safari hii ndefu, na bila kujali upungufu wake tunaweza kusema bila kusita kwamba lina nafasi yake katika historia ya mapambano ya binadamu yenye lengo la kuondokana na ushenzi ("barbarism") wa ubepari na kuelekea kwenye ustaarabu wa kisoshalisti.

# Sura ya Pili

## Azimio la Arusha

## Ujamaa na Kujitegemea

*(Lilipitishwa na Halmashauri Kuu ya TANU, mwezi Januari 1967, na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa TANU)*
*(Lilitolewa rasmi tarehe 5 Februari 1967)*

### SEHEMU YA KWANZA

**Imani ya Tanu**

Siasa ya TANU ni kujenga nchi ya Ujamaa. Misingi ya Ujamaa imetajwa katika Katiba ya TANU, nayo ni hii:

Kwa kuwa TANU inaamini:

(a) Kwamba binadamu wote ni sawa;
(b) Kwamba kila mtu anastahili heshima;
(c) Kwamba kila raia ni sehemu ya Taifa na anayo haki ya kushiriki sawa na wengine katika Serikali tangu ya Mitaa, ya Mikoa hadi Serikali Kuu;
(d) Kwamba kila raia anayo haki ya uhuru wa kutoa mawazo yake, wa kwenda anakotaka, wa kuamini dini anayotaka na wa kukutana na watu mradi havunji Sheria;
(e) Kwamba kila mtu anayo haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake na ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa Sheria;
(f) Kwamba kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake;
(g) Kwamba raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao;

(h) Kwamba ili kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi unakwenda sawa Serikali lazima iwe na mamlaka kamili juu ya njia muhimu za kuukuza uchumi; na

(i) Kwamba ni wajibu wa Serikali, ambayo ni watu wenyewe, kuingilia kati kwa vitendo maisha ya uchumi ya Taifa ili kuhakikisha usitawi wa raia wote na kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine au kikundi kimoja kunyonya kikundi kingine na kuzuia limbikizo la utajiri kufikia kiasi ambacho hakipatani na siasa ya watu wote kuwa sawa.

## Madhumuni ya Tanu

Kwa hiyo basi, makusudi na madhumuni ya TANU yatakuwa kama hivi yafuatavyo:

(a) Kuudumisha uhuru wa nchi yetu na raia wake;

(b) Kuweka heshima ya mwanadamu kwa kufuata barabara kanuni za Tangazo la Ulimwengu la Haki za Binadamu;

(c) Kuhakikisha kwamba nchi yetu inatawaliwa na Serikali ya watu ya kidemokrasia na ya kisoshalist;

(d) Kushirikiana na vyama vyote vya siasa katika Afrika vinavyopigania uhuru wa bara lote la Afrika;

(e) Kuona kwamba Serikali inatumia mali yote ya nchi yetu kwa kuondoshea umaskini; ujinga na maradhi;

(f) Kuona kwamba Serikali inasaidia kwa vitendo kuunda na kudumisha vyama vya ushirika;

(g) Kuona kwamba kila iwezekanapo Serikali inashiriki hasa katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu;

(h) Kuona kwamba Serikali inatoa nafasi zilizo sawa kwa wote, wake kwa waume, bila kujali rangi, kabila, dini au hali;

(i) Kuona kwamba Serikali inaondoa kila namna ya dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa na upotofu;

(j) Kuona kwamba Serikali ya nchi yetu inasimamia barabara njia kuu za kuzalisha mali na inafuata siasa ambayo itarahisisha njia ya kumiliki kwa jumla mali za nchi yetu;

(k) Kuona kwamba Serikali inashirikiana na dola nyingine katika Afrika

katika kuleta Umoja wa Afrika.

(l) Kuona kwamba Serikali inajitahidi kuleta amani na salama ulimwenguni kwa njia ya Chama cha Umoja wa Mataifa.

## SEHEMU YA PILI

### Siasa ya Ujamaa

***(a) Hakuna Unyonyaji***

Nchi yenye Ujamaa kamili ni nchi ya wafanyakazi: haina ubepari wala ukabaila. Haina tabaka mbili za watu: tabaka ya chini ya watu wanaoishi kwa kufanya kazi, na tabaka ya juu ya watu wanaoishi kwa kufanyiwa kazi. Katika nchi ya Ujamaa kamili mtu hamnyonyi mtu, bali kila awezaye kufanya kazi hufanya kazi, na kila mfanyakazi hupata pato la haki kwa kazi aifanyayo na wala mapato ya wafanyakazi mbalimbali hayapitani mno.

Katika nchi ya Ujamaa kamili watu peke yao ambao huishi kwa jasho la wenzao, na ni haki yao kuishi kwa jasho la wenzao, ni watoto wadogo, wazee wasiojiweza, vilema na wale ambao, kwa muda, Jumuia imeshindwa kuwapatia kazi yoyote ya kujipatia riziki kwa nguvu zao wenyewe.

Nchi yetu ni nchi ya Wakulima na Wafanyakazi, lakini si nchi ya Ujamaa kamili. Ina misingi ya ubepari na ukabaila na vishawishi vyake. Misingi hii ya ubepari na ukabaila yaweza ikapanuka na kuenea.

***(b) Njia Kuu za Uchumi ni Chini ya Wakulima na Wafanyakazi***

Namna ya pekee ya kujenga na kudumisha ujamaa ni kuthibitisha kuwa njia kuu zote za uchumi wa nchi yetu zinatawaliwa na kumilikiwa na Wakulima na Wafanyakazi wenyewe kwa kutumia vyombo vya Serikali yao na Vyama vyao vya Ushirika. Pia ni lazima kuthibitisha kuwa Chama kinachotawala ni Chama cha wakulima na wafanyakazi.

*Njia kuu za Uchumi ni:* kama vile ardhi, misitu, madini, maji, mafuta na nguvu za umeme; njia za habari, njia za usafirishaji; mabenki, na bima; biashara na nchi za kigeni na biashara za jumla; viwanda vya chuma, mashini, silaha, magari, simenti, mbolea; nguo, na kiwanda chochote kikubwa ambacho kinategemewa na sehemu kubwa ya watu katika kupata riziki zao au kinachotegemewa na viwanda vingine; mashamba makubwa na hasa yale yanayotoa mazao ya lazima katika viwanda vikubwa.

Baadhi ya njia hizi na nyingine zisizotajwa hapa hivi sasa zinamilikiwa au kutawaliwa na Serikali ya Wananchi.

***(c) Kuna Demokrasi***

Nchi haiwi ya Ujamaa kwa sababu tu njia zake kuu au zote za uchumi hutawaliwa na humilikiwa na Serikali. Sharti Serikali iwe inachaguliwa na kuongozwa na Wakulima na Wafanyakazi wenyewe. Serikali ya Makaburu wa Rhodesia au Afrika ya Kusini ikitawala au kumiliki njia zote za uchumi, hiyo itakuwa ni njia ya kukomaza Udhalimu siyo njia ya kuleta Ujamaa. Hakuna Ujamaa wa kweli pasipo na Demokrasi ya kweli.

***(d) Ujamaa ni Imani***

Lakini Ujamaa hauwezi kujijenga wenyewe. Kwani Ujamaa ni imani. Hauna budi kujengwa na watu wanaoamini na kufuata kanuni zake. Mwana-TANU wa kweli ni Mjamaa, na Wajamaa wenzie, yaani waamini wenzie katika imani hii ya kisiasa na uchumi ni wote wale wanaopigania haki za wakulima na wafanyakazi katika Afrika na popote duniani. Wajibu wa kwanza wa mwana-TANU na hasa kiongozi wa TANU, ni kutii kanuni hizi za ujamaa hasa katika maisha yake mwenyewe. Na hasa mwana-TANU kiongozi hataishi kwa jasho la mtu mwingine au kufanya jambo lolote ambalo ni la kibepari au kikabaila.

Utimizaji wa shabaha hizo na nyinginezo zinazofuatana na siasa ya ujamaa unategemea sana viongozi kwa sababu ujamaa ni imani na ni vigumu kwa viongozi kujenga siasa ya ujamaa ikiwa hawaikubali imani hiyo.

## SEHEMU YA TATU

### Siasa ya Kujitegemea

### Tunapigana Vita:

TANU ina vita vya kulitoa Taifa letu katika hali ya unyonge na kulitia katika hali ya nguvu; vita vya kuwafanya wananchi wa Tanzania (na wananchi wa Afrika) watoke katika hali ya dhiki na kuwa katika hali ya neema.

Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, na tumepuuzwa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe, na kupuuzwa. Sasa tunataka mapinduzi; mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena, tusinyonywe tena na wala tusipuuzwe tena.

### Mnyonge Hapigani kwa Fedha:

Lakini ni dhahiri kwamba tumefanya makosa katika kuchagua silaha; kwani silaha tuliyochagua ni fedha. Tunataka kuondoa unyonge wetu kwa kutumia silaha ya wenye nguvu, silaha ambayo sisi wenyewe hatuna. Katika mazungumzo yetu, mawazo yetu, na vitendo vyetu ni kama tumekata shauri kwamba bila fedha mapinduzi yetu hayawezekani. Ni kama tumesema, ‘Fedha ndiyo msingi wa maendeleo. Bila fedha hakuna maendeleo’!

Hii ndiyo imani yetu ya sasa. Viongozi wa TANU mawazo yao ni kwenye fedha. Viongozi wa Serikali, wanasiasa na watumishi, mawazo yao na matumaini yao ni kwenye fedha. Viongozi wa wananchi na wananchi wenyewe katika TANU, NUTA, Bunge, UWT, Vyama vya Ushirika, TAPA na makundi mengine ya wananchi, mawazo yao na maombi yao na matumaini yao ni FEDHA. Ni kama wote tumekubaliana na tunasema kwa sauti moja, ‘Tukipata fedha tutaendelea, bila fedha hatutaendelea’!

Mpango wetu wa maendeleo ya miaka mitano shabaha zake kwa kifupi ni shibe zaidi, elimu zaidi na afya zaidi. Na silaha yetu tuliyotilia mkazo sana

ni fedha. Ni kama tumesema, ‘Katika miaka mitano ifuatayo tunakusudia kujiongezea shibe, elimu na afya, na ili kutimiza shabaha hizo tunatumia £ 250,000,000’. Kama tumetaja na tunapotaja vyombo vingine vya kututimizia shabaha hizo tunavitaja kama nyongeza tu; lakini chombo kikubwa katika akili zetu, silaha kubwa katika mawazo yetu, ni FEDHA.

Mheshimiwa Mbunge anaposema kuwa wananchi wa sehemu yake wana shida ya maji, je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa shida hiyo? Jibu analotaka ni kwamba: Serikali inao mpango wa kuwapa maji wananchi wa sehemu hiyo – KWA FEDHA.

Mbunge mwingine anaposema kuwa sehemu yake haina barabara au shule au hospitali au vyote, je, Serikali ina mpango gani? Naye pia jibu ambalo angependa kupewa ni kuwa Serikali inao mpango safi kabisa wa kutengeneza barabara au kujenga shule au hospitali au vyote kwa wananchi wa sehemu ya Mbunge Mheshimiwa huyo – kwa FEDHA.

Kiongozi wa NUTA anapoikumbusha Serikali kuwa mishahara ya chini kwa wafanyakazi wengi bado ni midogo mno na nyumba wanazolala si nzuri, je, Serikali inao mpango gani? Jibu apendalo kusikia ni kuwa Serikali inao mpango maalum wa kuongeza mishahara na kujenga majumba bora – KWA FEDHA.

Kiongozi wa TAPA anaposema kuwa wanazo shule nyingi sana ambazo hazipati msaada wa Serikali, je, Serikali ina mpango gani wa kuzisaidia shule hizo, jibu analopenda kusikia ni kuwa Serikali iko tayari kabisa kesho asubuhi kuzipa shule hizo msaada unaotakiwa – wa FEDHA!

Kiongozi wa Chama cha Ushirika akitaja shida yoyote ya mkulima jibu apendalo kusikia ni kuwa Serikali itaondoa shida hizo za mkulima – kwa FEDHA. Mradi kila shida inayolikabili Taifa letu wananchi tunawaza Fedha, Fedha, Fedha!

Mwaka hata mwaka kila Wizara na kila Waziri hufanya makadirio yake ya matumizi – yaani fedha wanazohitaji mwaka huo kwa kazi za kawaida na mipango ya maendeleo. Waziri mmoja tu na Wizara moja tu hushughulika pia kufanya makadirio ya mapato. Ni Waziri wa Fedha. Kila Wizara ina mipango mizuri sana ya maendeleo. Wizara zinapoleta makadirio yao ya matumizi huwa zinaamini kwamba fedha zipo ila mkorofi ni Waziri wa Fedha na Wizara yake. Na kila mwaka lazima Waziri wa Fedha na Wizara yake awaambie Mawaziri wenzake na Wizara zao kwamba hakuna fedha. Na kila mwaka Wizara zote huinung'unikia Wizara ya Fedha kwa kupunguza Makadirio yao ya matumizi.

Kadhalika Wabunge na Viongozi wengine wanapodai Serikali itimize mipango mbalimbali huwa nao wakiamini kwamba fedha zipo ila mkorofi ni Serikali. Lakini kukataa huku kwa Wizara, na Wabunge na Viongozi wengine hakuwezi kuondoa ukweli; nao ni kwamba Serikali haina fedha.

Na kusema kuwa Serikali haina fedha maana yake ni nini? Maana yake ni kuwa Wananchi wa Tanzania hawana fedha. Kiasi walichonacho hutozwa kodi, na kodi hiyo ndiyo inayoendesha shughuli za Serikali hivi sasa na maendeleo mengine ya nchi. Tunapotaka Serikali ifanye shughuli zaidi za maendeleo kwa fedha tunataka Serikali itumie fedha zaidi. Na kama Serikali haina fedha zaidi tunataka izipate, yaani iongeze kodi.

Ukidai Serikali itumie fedha zaidi unataka izipate; na njia ya kuzipata ni kodi. Kudai Serikali itumie fedha nyingi zaidi bila kukubali kodi zaidi ni kudai Serikali ifanye miujiza; ni sawa na kudai maziwa zaidi bila kutaka ng'ombe akamuliwe tena. Lakini kukataa huku kukiri kwamba tunapodai Serikali itumie fedha zaidi nia yetu ni kutaka Serikali iongeze kodi kunaonyesha kuwa tunatambua ugumu wa kuongeza kodi. Tunatambua kuwa ng'ombe hana maziwa zaidi; kwamba hata kama ng'ombe mwenyewe angependa ayanywe maziwa hayo au yanywewe na ndama wake au yauzwe yamfae yeye na jamaa yake; utashi huo hauwezi kuondoa ukweli kwamba hana maziwa zaidi.

## Fedha kutoka Nje ya Tanzania, Je?

Njia moja tunayotumia kujaribu kuepukana na lazima hii ya kukiri kodi zaidi ikiwa twataka fedha zaidi ni kutilia sana mkazo fedha za kutoka nje ya Tanzania. Fedha hizi za kutoka nje ni za aina tatu:-

*(a)* ***Zawadi***: Yaani Serikali ya nje iipe Serikali yetu fedha za bure tu kama sadaka kwa ajili ya mpango fulani wa maendeleo. Wakati mwingine shirika lolote la nje liipe Serikali yetu au Shirika jingine katika nchi yetu msaada fulani kwa ajili ya maendeleo.

*(b)* ***Mkopo:*** Sehemu kubwa ya fedha tunazotazamia kupata kutoka nchi za kigeni si zawadi au sadaka, bali ni mkopo. Serikali ya nje au Shirika la nje, kama vile Benki, hukopesha Serikali yetu fedha fulani kwa ajili ya kazi zetu za maendeleo. Mkopo huu huwa una masharti yake ya kulipa, kama vile muda wa kulipa, na kima cha faida.

*(c)* ***Raslimali ya Kibiashara:*** Aina ya tatu ambayo pia ni kubwa kuliko ya kwanza, ni ile ya fedha za watu au makampuni yanayotaka kuja katika nchi yetu kuanzisha shughuli mbalimbali za uchumi kwa manufaa yao wenyewe. Na sharti kubwa walitakalo jamaa hawa wenye fedha zao ni kwamba shughuli yenyewe iwe ni ya faida – kwao – na pia kwamba Serikali iwaruhusu kuondoa faida hiyo Tanzania na kuipeleka kwao. Hupenda pia kwa jumla Serikali iwe na siasa wanayokubaliana nayo au ambayo haihatarishi uchumi wao.

Hizo ndizo njia tatu kubwa za kupata fedha kutoka nje ya nchi yetu. Kuna mazungumzo mengi ajabu juu ya jambo hili la kupata fedha kutoka nchi za kigeni. Serikali yetu na viongozi wetu wa makundi mbalimbali hawaachi kufikiria njia za kupata fedha kutoka nje. Na tukizipata au japo tukipata ahadi tu ya kuzipata mara magazeti yetu, au radio zetu na viongozi wetu hutangaza jambo hilo ili kila mtu ajue kuwa neema imekuja au iko njiani inakuja! Tukipata msaada hutangaza; tukipata mkopo hutangaza; tukipata kiwanda kipya hutangaza; tukiahidiwa msaada, mkopo au kiwanda kipya hutangaza. Japo tukianza mazungumzo tu na nchi au shirika la kigeni juu ya msaada, mkopo au kiwanda, mara hutangaza japo hatuna hakika ya matokeo

ya mazungumzo hayo. Na kisa? Ni kuwajulisha wananchi kwamba, tunaanza mazungumzo ya neema!

## Tusitegemee Fedha Kuleta Maendeleo

Ni jambo la kijinga kuchagua fedha kuwa ndiyo chombo chetu kikubwa cha maendeleo na hali tunajua kuwa nchi yetu ni maskini. Ni ujinga vilevile, kwa kweli ni ujinga zaidi, tukidhani kuwa tunaweza kuondoa hali hii ya unyonge wetu kwa kutegemea fedha za kutoka nje badala ya fedha zetu wenyewe. Ni ujinga kwa sababu mbili.

Kwanza, hatuwezi kuzipata. Ni kweli kwamba zipo nchi ambazo zaweza na zapenda kutusaidia. Lakini hakuna nchi moja duniani ambayo iko tayari kutupa misaada au mikopo au kuja kujenga viwanda katika nchi yetu kwa kiasi cha kuiwezesha nchi yetu kutimiza shabaha zake zote za maendeleo. Nchi zenye dhiki ni nyingi sana duniani. Na hata kama nchi zote zenye neema zingekubali kuzisaidia nchi zenye dhiki, bado ingekuwa msaada huo hautoshi. Lakini nchi zenye neema hazitakubali. Hata katika nchi ileile, matajiri huwa hawatoi fedha zao kwa hiari ili zisaidie Serikali kuondoa dhiki.

Njia ya kuzipata fedha za matajiri ili zisaidie umma ni kuwatoza kodi wakipenda wasipende. Hata hivyo huwa hazitoshi. Ndiyo maana japo tungewakamua vipi wanananchi na wakazi wa Tanzania, matajiri na maskini, hatuwezi kupata fedha za kutosha kutimiza mipango yetu ya maendeleo. Wala duniani hakuna Serikali ambayo yaweza kuyatoza kodi mataifa yenye neema, yakipenda yasipende, ili kusaidia mataifa yenye dhiki. Hata hizo zisingelitosha. Hakuna Serikali ya Dunia nzima. Fedha ambazo nchi zenye neema hutoa huwa kwa wema wao, au hiari yao au kwa manufaa yao wenyewe. Haiwezekani basi, tupate fedha za kutosha kwa njia hiyo.

## Misaada na Mikopo Vitahatarisha Uhuru Wetu

Pili, japo kama tungeweza kuzipata; hivyo ndivyo tunavyotaka kweli? Kujitawala ni kujitegemea. Kujitawala kwa kweli hakuwezekani ikiwa Taifa moja linategemea misaada na mikopo ya Taifa jingine kwa maendeleo yake. Hata kama pangetokea Taifa au mataifa ambayo yako tayari kutupa fedha

zote tunazohitaji kuendesha mipango yetu ya maendeleo isingekuwa sawa kwa nchi yetu kuipokea misaada hiyo bila kujiuliza matokeo yake yatakuwa nini kwa Uhuru wetu na uzima wetu.

Msaada ambao ni kama chombo cha kuongeza juhudi, au nyenzo ya juhudi, ni msaada ambao una manufaa. Lakini msaada unaoweza ukawa sumu ya juhudi si msaada wa kupokea bila kujiuliza maswali.

Kadhalika mikopo. Kweli mkopo ni bora kuliko misaada ya 'bure'. Mkopo nia yake ni kuongeza jitihada au kuifanya jitihada itoe matunda mengi zaidi. Sharti moja la mkopo huwa ni kuonyesha jinsi utavyoweza kuulipa. Maana yake ni kwamba sharti uonyeshe kuwa unakusudia kuufanyia kazi itakayoleta manufaa ya kukuwezesha kuulipa.

Lakini hata mikopo ina kikomo. Sharti upime uwezo wa kulipa. Tunapokopa fedha kutoka nje mlipaji ni Mtanzania. Na kama tulivyokwishasema Watanzania ni watu maskini. Kuwabebesha watu maskini mikopo ambayo inawazidi kimo si kuwasaidia bali ni kuwaumiza. Na hasa inapokuwa, mikopo hiyo ambayo wanatakiwa walipe, haikuwafaidia wao, bali ilifaidia watu wachache tu.

*Na Viwanda vya wenye raslimali zao je?* Ni kweli tunavitaka. Hata tumepitisha katika Bunge sheria ya kulinda raslimali ya wageni wanaoanzisha mipango mbalimbali ya uchumi katika nchi yetu. Nia yetu na matumaini yetu ni kuwafanya waone kuwa Tanzania ni nchi inayofaa kuingiza raslimali zao. Kwani raslimali yao itakuwa salama italeta faida. Na faida hiyo wenyewe wataweza kuiondoa bila vipingamizi. Tunayo matumaini ya kupata fedha za maendeleo mbalimbali kwa njia hii. Lakini hatuwezi kupata za kutosha. Lakini hata kama tungeweza kuwaridhisha kabisa Wageni hao na Makampuni hayo mpaka yakubali kuanzisha mipango yote ya uchumi tunayohitaji katika nchi yetu, hivyo ndivyo tunavyotaka kweli?

Kama tungeweza kushawishi wenye raslimali wa kutosha kutoka Amerika, na Ulaya kuja kwetu na kuanzisha Viwanda vyote, na mipango mingine yote ya uchumi tunayohitaji katika nchi hii, hivi kweli tungekubali bila kujiuliza maswali? Tungekubali kweli kuacha uchumi wetu wote uwe mikononi mwa wageni kwa ajili ya kupata faida na kuipeleka katika nchi zao? Hata kama wasingedai kuhamisha faida na kupeleka makwao, bali faida yote watakayopata wataitumia hapa hapa Tanzania kwa maendeleo zaidi. Hivi kweli tungekubali jambo hili bila kujiuliza hasara zake kwa Taifa letu? Huu Ujamaa tunaosema kuwa ndiyo shabaha yetu tungeujengaje?

Twawezaje kutegemea nchi za nje na Kampuni za nje kwa misaada na mikopo na raslimali kwa maendeleo yetu bila kuhatarisha uhuru wetu? Waingereza wana methali isemayo 'Amlipaye mwimbaji ndiye huchagua wimbo'. Tutawezaje kutegemea nchi za kigeni na Makampuni ya kigeni kwa sehemu kubwa ya maendeleo yetu bila kuzipa nchi hizo na makampuni hayo sehemu kubwa ya uhuru wetu wa kutenda tupendavyo? Ukweli wenyewe ni kwamba hatuwezi.

Tukariri basi. Tumefanya makosa kuchagua fedha, kitu ambacho hatuna, kiwe ndicho chombo kikubwa cha mipango yetu ya maendeleo. Tunafanya makosa kudhani kuwa tutapata fedha kutoka nchi za kigeni. Kwanza, kwa sababu kwa kweli hatuwezi kupata fedha za kutosha kwa maendeleo yetu. Na pili, hata kama tungeweza, huko kutegemea wengine kungehatarisha uhuru wetu na siasa nyingine za nchi yetu.

## Tumekazania Mno Viwanda

Kwa sababu ya kutilia mkazo fedha tumefanya kosa kubwa la pili. Tumekazania mno viwanda. Kama vile tulivyosema 'Bila Fedha hakuna maendeleo', ni kama twasema pia 'Viwanda ndiyo maendeleo. Bila viwanda hakuna maendeleo'. Hii ni kweli siku tutakapokuwa na fedha nyingi, tutaweza kusema kwamba tumeendelea. Tutaweza kusema, 'Tulipoanza mipango yetu tulikuwa hatuna fedha za kutosha na upungufu huu wa fedha ulitupunguzia nguvu za kuendesha maendeleo yetu haraka zaidi. Lakini leo tumeendelea na tunazo fedha za kutosha'. Na hivyo ndivyo itakavyotupasa kusema, 'Tumeendelea,

*kwa hiyo*, tunazo fedha za kutosha'. Yaani fedha zetu zitakuwa zimeletwa na maendeleo.

Kadhalika siku tutakapokuwa na viwanda tuna haki ya kusema kuwa tumeendelea. Maendeleo yatakuwa yametuwezesha kupata viwanda. Kosa tunalofanya ni kudhani kwamba maendeleo yetu yataanza kwa viwanda. Ni kosa maana hatuna uwezo wa kuanzisha viwanda vingi vya kisasa katika nchi yetu. Hatuna fedha zinazohitajiwa na hatuna ufundi unaohitajiwa. Haitoshi kusema kuwa tutakopa fedha na kuazima mafundi kutoka nje kuja kuanzisha viwanda hivyo. Kosa hili jibu lake ni lilelile kwamba hatuwezi kupata fedha za kutosha na kuazima mafundi wa kutosha kutuanzishia viwanda hivyo tunavyotaka. Na pia kwamba hata kama tungeweza kupata msaada huo kuutegemea huko kunaweza kukapotosha siasa yetu ya Ujamaa. Siasa ya kualika msululu wa mabepari kuja kuhodhi viwanda katika nchi yetu ingefanikiwa kutupatia viwanda vyote tunavyotaka, basi ingefanikiwa pia kuzuia maendeleo ya Ujamaa. Ila labda tuwe tunaamini kwamba bila kujenga ubepari kwanza hatuwezi kujenga Ujamaa.

## Tumjali Zaidi Mkulima Vijijini

Vilevile mkazo wa fedha na wa viwanda unatufanya tukazanie zaidi maendeleo ya mijini. Tunatambua kuwa hatuwezi kupata fedha za kutosha kuleta maendeleo katika kila kijiji na ambayo yatamfaa kila mwananchi. Tunajua pia kuwa hatuwezi kujenga kiwanda katika kila kijiji ili kisaidie kuleta maendeleo ya fedha na viwanda katika kila kijiji; jambo ambalo tunajua kuwa haliwezekani. Kwa ajili hiyo, basi, fedha zetu huzitumia zaidi katika miji na viwanda vyetu pia hujengwa katika miji.

Na zaidi ya fedha hizi huwa ni mikopo. Japo zijenge shule, hospitali, majumba au viwanda ni fedha za mikopo. Hatimaye lazima zilipwe. Lakini ni dhahiri kwamba haziwezi kulipwa kwa fedha zinazotokana na maendeleo ya mijini au maendeleo ya viwanda. Hazina budi zilipwe kwa fedha tunazopata kutokana na vitu tunavyouza katika nchi za nje. Kutokana na viwanda vyetu hatuuzi na kwa muda mrefu sana hatutauza vitu vingi katika nchi za nje. Viwanda

vyetu zaidi ni vya kutusaidia kupata vitu hapa hapa ambavyo mpaka sasa tunaviagiza kutoka nchi za nje. Itapita miaka mingi kabla ya kuweza kuuza katika nchi za nje vitu vinavyotokana na viwanda vyetu.

Kwa hiyo ni dhahiri kwamba fedha tutakazotumia kulipa madeni haya ya mikopo ya fedha kwa maendeleo na viwanda mijini hazitatoka mijini na wala hazitatokana na viwanda. Zitatoka wapi, basi? Zitatoka vijijini na zitatokana na KILIMO. Maana ya ukweli huu ni nini? Ni kwamba wale wanaofaidi maendeleo yanayotokana na fedha tunazokopa sio kwa kweli watakaozilipa. Fedha zitatumika zaidi katika miji lakini walipaji watakuwa zaidi ni wakulima.

Jambo hili linafaa kukumbukwa sana, maana kuna njia nyingi za kunyonyana. Tusisahau hata kidogo kwamba wakaaji wa mijini wanaweza wakawa wanyonyaji wa jasho la wakulima wa vijijini. Hospitali zetu kubwa zote ziko katika miji. Zinafaidia sehemu ndogo sana ya wananchi wa Tanzania. Lakini kama tumezijenga kwa fedha za mkopo walipaji wa mkopo ni wakulima, yaani wale ambao hawafaidiwi sana na hospitali hizo. Mabarabara ya lami yako katika miji, kwa faida ya wakaaji wa mijini na hasa wenye magari. Kama mabarabarabara hayo tumeyajenga kwa fedha za mikopo walipaji ni wakulima; na fedha zilizonunua magari yenyewe zilitokana na mazao ya wakulima. Taa za umeme, maji ya mabomba, mahoteli na maendeleo mengine yote ya kisasa yako zaidi katika miji. Karibu yote yametokana na fedha za mikopo na karibu yote hayana faida kubwa kwa mkulima, lakini yatalipwa kwa fedha zitakazotokana na jasho la mkulima. Tusisahau jambo hili.

Japo tunapotaja unyonyaji hufikiria mabepari, tusisahau kuwa bahari ina samaki wengi. Nao hutafunana. Mkubwa hutafuna mdogo na mdogo naye humtafuna mdogo zaidi. Katika nchi yetu twaweza kugawa wananchi kwa njia mbili. Mabepari na Makabaila upande mmoja; na wafanyakazi na wakulima upande mwingine. Pia twaweza tukawagawa wakaaji wa mijini upande mmoja, na wakulima wa vijijini upande mwingine. Tusipoangalia tutakuja kugundua kuwa wakaaji wa mijini nao ni wanyonyaji wa wakulima.

## Wananchi na Kilimo

Maendeleo ya nchi huletwa na watu, hayaletwi na fedha. Fedha ni matokeo siyo msingi wa maendeleo. Ili tuendelee twahitaji vitu vinne: (i) Watu; (ii) Ardhi; (iii) Siasa safi na (iv) Uongozi bora. Nchi yetu ina zaidi ya watu milioni kumi[2] na eneo la eka 362,000.

## Maendeleo Yataletwa na Kilimo

Sehemu kubwa ya eneo hili ni yenye rutuba na mvua ya kutosha. Nchi yetu inaweza kutoa mazao ya aina mbalimbali ambayo tunayahitaji kwa chakula na kwa fedha. Mazao ya chakula (na fedha kama tukiyatoa kwa wingi) ni kama vile mahindi, mchele, ngano, maharage, karanga n.k. Mazao ya fedha ni kama vile mkonge, pamba, kahawa, tumbaku, pareto, chai n.k.

Pia nchi yetu ni nzuri sana kwa ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku n.k. Pia twaweza kuvua samaki katika maziwa, bahari na mito.
Wakulima wetu wako katika sehemu ambazo zaweza kutoa mazao haya, kama si yote walau mawili matatu au hata zaidi. Kila mkulima wetu aweza akaongeza mazao haya ili ajipatie chakula kingi zaidi au fedha nyingi zaidi. Na kwa sababu nia kubwa ya maendeleo ni kupata chakula zaidi na fedha zaidi kwa ajili ya kujipatia mahitaji yetu mengine, ndiyo kusema kuwa jitihada ya kuongeza mazao ni jitihada, na kwa kweli ndiyo jitihada peke yake, ambayo italeta maendeleo, yaani chakula zaidi na fedha zaidi kwa kila mwananchi.

## Masharti ya Maendeleo

### *(a) Juhudi*

Kila mwananchi anataka maendeleo, lakini si kila mwananchi anaelewa na kukubali masharti ya maendeleo. Sharti moja kubwa ni JUHUDI. Twendeni vijijini tuzungumze na wananchi kuona kama inawezekana au haiwezekani wananchi kuongeza juhudi.
Kwa mfano, katika miji, mfanyakazi wa mshahara hufanya kazi kwa saa saba na nusu au nane kutwa kwa muda wa siku sita au sita na nusu kwa juma.

---
[2] Hesabu ya watu ya mwaka 1967 ilionesha kuwa watanzania ni zaidi ya milioni kumi na mbili.

Tuseme saa 45 kwa juma, kuondoa majuma mawili au matatu ya livu, katika mwaka mzima. Ndiyo kusema mfanyakazi wa mjini hufanya kazi ya saa 45 kwa juma kwa majuma 48 au 50 kwa mwaka.

Katika nchi kama yetu muda huu ni mdogo kwa kweli. Nchi nyingi hata zilizoendelea kutuzidi – hufanya kazi kwa muda mrefu zaidi kuliko saa 45 kwa juma. Si jambo la kawaida nchi changa kuanza na muda mfupi kama huo. Jambo la kawaida ni kuanza na muda mrefu zaidi na kuupunguza kila nchi inavyozidi kuendelea. Sisi kwa kuanza na muda mfupi huu na tunapodai muda mfupi zaidi kwa kweli tunaiga nchi zilizoendelea. Na kuiga huku kunaweza kukaleta majuto. Lakini hata hivyo wafanyakazi wa mishahara hufanya kazi ya saa 45 kwa juma; livu yao kwa mwaka haizidi majuma manne.

Yafaa kujiuliza wananchi wakulima hasa wanaume, hufanya kazi kwa saa ngapi kwa juma na miezi mingapi kwa mwaka. Ni wengi mno ambao hawatimizi hata nusu ya wastani wa mfanyakazi wa mshahara.

Ukweli wenyewe ni kwamba vijijini kina mama hufanya sana kazi. Pengine hutimiza saa 12 au 14 kutwa. Hawana Jumapili, na hawana livu. Kina mama wa vijijini hufanya kazi zaidi kuliko mtu mwingine yeyote katika Tanzania. Lakini kina baba wa vijijini (na baadhi ya kina mama wa mijini) nusu ya maisha yao ni livu. Nguvu hizi za mamilioni ya kina baba vijijini na maelfu ya kina mama wa mijini ambazo hivi sasa hazifanyi kazi yoyote ila kupiga soga, kucheza ngoma na kunywa pombe, ni hazina kubwa yenye manufaa zaidi kwa maendeeo ya nchi yetu kuliko hazina za mataifa matajiri.

Tutafanya jambo la faida kubwa kwa nchi yetu kama tukienda vijijini na kuwaambia wananchi kwamba wanayo hazina hii na kwamba ni wajibu wao kuitumia kwa faida yao wenyewe na faida ya Taifa letu.

***(b) Maarifa***

Sharti la pili la maendeleo ni MAARIFA. Juhudi bila maarifa haiwezi kutoa matunda bora kama juhudi na maarifa. Kutumia jembe kubwa badala ya

jembe dogo, kutumia jembe la kuvutwa na ng'ombe badala ya jembe la mkono, kutumia mbolea badala ya ardhi tupu, kunyunyizia dawa ili kuua wadudu, kujua ni zao gani lifaalo kupandwa na zao gani lisilofaa, kuchagua mbegu vizuri kabla ya kuzipanda, kujua wakati mzuri wa kupanda, wakati wa kupalilia n.k., ni maarifa yanayowezesha juhudi kutoa mazao mengi zaidi.

Fedha na wakati tunaotumia kuwapa wakulima maarifa haya ni fedha na wakati uletao faida kubwa zaidi kwa nchi yetu kuliko fedha na wakati mwingi tunaotumia katika mambo mengi tunayoyaita maendeleo.

Jambo hili kwa kweli tunalifahamu. Katika mpango wetu wa miaka mitano, mipango inayoendelea vizuri na hata kuzidi makisio ni ile inayotegemea juhudi ya wananchi wenyewe. Pamba, kahawa, korosho, tumbaku, pareto ni mazao yaliyoongezeka kwa haraka sana katika muda wa miaka mitatu iliyopita. Lakini ni mazao ambayo yameongezeka kwa sababu ya juhudi na uongozi wa wananchi, siyo kwa sababu ya fedha.

Kadhalika wananchi kwa juhudi zao wenyewe na maelekezo au msaada kidogo wametimiza mipango mingi sana ya maendeleo huko vijijini. Wamejenga shule, dispensari, majumba ya maendeleo, wamechimba visima, mifereji ya maji, mabwawa, mabarabara, wamejenga mabirika ya kukoshea mifugo na kujiletea wenyewe maendeleo ya aina mbalimbali. Kama wangengoja fedha wasingeyapata maendeleo hayo.

## Juhudi ni Shina la Maendeleo

Mipango inayotegemea fedha inakwenda vizuri lakini kuna mingi ambayo imesimama na yumkini mingine haitatimizwa kwa sababu ya upungufu wa fedha. Lakini kelele zetu bado ni kelele za fedha. Juhudi yetu ya kutafuta fedha inazidi kuongezeka! Sio kwamba tuipunguze, bali, badala ya safari nyingi, ndefu na zenye gharama kubwa za kwenda katika miji mikuu ya mataifa ya kigeni kwenda kutafuta fedha za maendeleo yetu, itafaa kufunga safari kwenda vijijini kuwafahamisha na kuwaongoza wananchi katika kujiletea maendeleo kwa juhudi yao wenyewe. Ndiyo njia ya kweli ya kuleta maendeleo kwa kila mtu.

Hii maana yake si kwamba tangu sasa hatutajali fedha, wala hatutajenga viwanda au kufanya mipango yoyote ya maendeleo inayohitaji fedha. Wala siyo kusema kuwa tangu sasa hatutapokea wala kutafuta fedha kutoka nchi za nje kwa ajili ya maendeleo yetu. LA, SIVYO. Tutaendelea kutumia fedha; na mwaka hata mwaka tutatumia fedha nyingi zaidi kwa maendeleo yetu ya aina mbalimbali kuzidi mwaka uliopita. Kwani hiyo itakuwa ni dalili moja ya maendeleo yetu.

Lakini hii ni kusema kwamba tangu sasa tutajua nini ni shina na nini ni tunda la maendeleo yetu. Katika vitu viwili hivyo FEDHA na WATU, ni dhahiri kwamba watu na JUHUDI yao ndiyo shina la maendeleo, fedha ni moja ya matunda ya juhudi hiyo.

Tangu sasa tutasimama wima na kutembea kwa miguu yetu badala ya kupinduka na kuwa miguu juu vichwa chini. Viwanda vitakuja, na fedha zitakuja, lakini msingi wake ni WANANCHI na JUHUDI yao na hasa katika KILIMO. Hii ndiyo maana ya kujitegemea. Kwa hiyo basi, mkazo wetu na uwe:

(l) Ardhi na Kilimo.
(m) Wananchi.
(n) Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, na
(o) Uongozi bora.

### *(a) Ardhi*

Kwa kuwa uchumi wa Tanzania unategemea na utaendelea kutegemea kilimo na mifugo, Watanzania wanaweza kuyaendesha maisha yao barabara bila ya kutegemea misaada kutoka nje kwa matumizi bora ya ardhi hiyo. Ardhi ni ufunguo wa maisha ya binadamu kwa hiyo Watanzania wote waitumie ardhi kama ni raslimali yao kwa maendeleo ya baadaye. Kwa kuwa Ardhi ni mali ya Taifa, Serikali ni lazima iangalie kuwa ardhi inatumiwa kwa faida ya Taifa zima na wala isitumiwe kwa faida ya mtu binafsi au kwa watu wachache tu. Ni wajibu wa TANU kuona kuwa nchi yetu inalima chakula cha kutosha na kutoa mazao ambayo yataleta fedha nchini kwa kuuzwa katika nchi

za ng'ambo. Ni wajibu wa Serikali na Vyama vya Ushirika kuona kuwa wananchi wanapatiwa vyombo, mafunzo ya uongozi unaohitajika katika kilimo na ufugaji wa kisasa.

### *(b) Watu*

Kuiwezesha siasa ya kujitegemea itekelezwe vizuri, wananchi ni budi wajengwe moyo na shauku ya kujitegemea. Wajitegemee katika kuwa na chakula cha kutosha, mavazi ya kufaa na mahali pazuri pa malazi.

Katika nchi yetu kazi iwe ni kitu cha kujivunia. Bali uvivu, ulevi na uzururaji uwe ni jambo la aibu kwa kila mwananchi. Katika upande wa ulinzi wa Taifa, wananchi wawe macho na vibaraka waliomo nchini ambao wanaweza kutumiwa na maadui wa nje wenye nia mbaya ya kuliangamiza Taifa hili na wawe tayari kulilinda Taifa inapolazimika kufanya hivyo.

### *(c) Siasa Safi*

Msingi wa siasa ya kujitegemea lazima uambatane na siasa ya Ujamaa ya TANU. Ili kuzuia unyonyaji ni lazima kila mtu afanye kazi na aishi kwa jasho lake yeye mwenyewe. Na ili kuleta usawa wa kugawana mapato ya nchi ni lazima kila mtu atimize wajibu wake kwa kufanya kazi kwa bidii zake zote. Asiweko mtu wa kwenda kwa ndugu yake na kukaa kwa muda mrefu bila kufanya kazi kwa sababu atakuwa anamnyonya yule ndugu yake. Vilevile mtu yeyote asiruhusiwe kuzurura zurura hovyo mijini au vijijini bila kufanya kazi ya kumwezesha kujitegemea mwenyewe bila kuwanyonya ndugu zake.

TANU inaamini kuwa kila anayelipenda Taifa lake ni budi aweze kulitumikia kwa kujitolea nafsi yake na kushirikiana na wananchi wenzake kwa kuijenga nchi kwa manufaa ya watu wote. Ili kudumisha Uhuru wa nchi yetu na raia zake barabara ni budi kujitegemea kwa kila hali bila kwenda kuomba misaada nchi zingine.

Kujitegemea kwa mtu mmoja ni kujitegemea kwa nyumba kumi. Kujitegemea kwa nyumba zote kumi za balozi ni kujitegemea kwa tawi zima. Kujitegemea kwa matawi ni kujitegemea kwa Wilaya ambayo ni kujitegemea kwa Mkoa.

Kujitegemea kwa Mikoa yote ni kujitegemea kwa Taifa lote ambalo ndilo lengo letu.

***(d) Uongozi Bora***

TANU inatambua umuhimu wa kuwa na Uongozi Bora. Tatizo lililopo ni ukosefu wa mipango maalum ya kuwafundisha Viongozi na kwa hiyo Ofisi Kuu ya TANU ni budi itengeneze utaratibu maalum kuhusu mafundisho ya Viongozi tangu wa Taifa zima hadi Mabalozi ili waielewe siasa yetu na mipango ya uchumi. Viongozi ni lazima wawe mfano mzuri kwa wananchi kwa maisha yao na vitendo vyao pia.

## SEHEMU YA NNE

### Uanachama

Tangu Chama kilipoanzishwa, tumethamini sana kuwa na wanachama wengi iwezekanavyo. Hii ilifaa wakati wa kupigania vita vya kumng'oa mkoloni. Hivyo ndivyo ilivyobidi TANU kufanya kwa wakati huo. Lakini sasa Halmashauri Kuu inaona kuwa wakati umefika wa kutilia mkazo kwenye imani ya Chama chetu na siasa yake ya Ujamaa.

Kifungu cha Katiba ya TANU kinachohusu uingizaji wa mtu kwenye Chama kifuatwe na ikiwa inaonekana kuwa mtu haelekei kuwa anakubali imani, madhumuni na sheria na amri za Chama, basi asikubaliwe kuingia. Na hasa isisahauliwe kuwa TANU ni Chama cha wakulima na wafanyakazi.

## SEHEMU YA TANO

### Azimio la Arusha

Kwa hiyo basi, Halmashauri Kuu ya Taifa iliyokutana katika Community Centre ya Arusha kuanzia tarehe 26/1/67 mpaka 29/1/67, inaazimia ifuatavyo:

**A. Viongozi**

1. Kiongozi wa TANU au wa Serikali sharti awe mkulima au mfanyakazi na asishiriki katika jambo lolote la kibepari au kikabaila.
2. Asiwe na hisa katika makampuni yoyote.
3. Asiwe mkurugenzi katika kampuni ya kikabaila au kibepari.
4. Asiwe na mishahara miwili au zaidi
5. Asiwe na nyumba ya kupangisha.
6. Viongozi tunaofikiria hapa ni wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Vyama vilivyoshirikishwa na TANU, Wakuu wa Mashirika ya Kiserikali, Viongozi kutokana na kifungu chochote cha Katiba ya TANU, Madiwani, na Watumishi wa Serikali wenye vyeo vya kati na vya juu. (Kwa mujibu wa kifungu hiki kiongozi ni mtu au mtu na mkewe au mke na mumewe).

**B. Serikali na Vyombo Vingine**

7. Inaipongeza Serikali kwa hatua zote ilizokwishachukua mpaka hivi sasa katika kutimiza siasa ya Ujamaa.
8. Inaihimiza Serikali, bila kungojea Tume ya Ujamaa, ichukue hatua zaidi za kutimiza siasa yetu ya Ujamaa kama ilivyoelezwa katika Tamko la TANU juu ya Ujamaa.
9. Inahimiza Serikali kutengeneza mipango yake kwa kutegemea uwezo wa nchi hii kuiendesha mipango hiyo na wala isitegemee mno mikopo na misaada ya nchi za ng'ambo kama ilivyofanya katika mpango wa maendeleo ya miaka mitano. Halmashauri Kuu ya Taifa inaazimia mpango huo urekebishwe ili ulingane na siasa ya kujitegemea.
10. Serikali ione kuwa mapato ya wafanyakazi nje ya Serikali hayapitani mno na yale ya wafanyakazi Serikalini.
11. Serikali itilie mkazo sana njia za kuinua maisha ya wakulima.
12. Inahimiza NUTA, Vyama vya Ushirika, TAPA, UWT, TYL, mashirika yote ya Serikali, kuchukua hatua ili kutekeleza siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

**C. Uanachama**

Wanachama wafundishwe kwa ukamilifu imani ya TANU ili waielewe, na wakumbushwe wakati wote umuhimu wa kuishika imani hiyo.

# Sura ya Tatu

# Azimio ni Matumaini ya Waliowengi

*Julius J.K Nyerere*

*[**Utangulizi wa wahiriri**: Mnamo mwezi Mei 1989, kulikuwa na semina ya wazalishaji wakubwa, wakiwemo wafanyabiashara binafsi na wakuu wa mashirika ya umma. Semina iliandaliwa na Chama ili kubadilishana mawazo juu ya masuala mbali mbali. Katika kipindi hiki cha awamu ya pili, chini ya Urais wa Mzee Ali Hassan Mwinyi, vuguvugu la kuachana na Azimio la Arusha tayari lilianza kujitokeza. Wakati wa kufunga Semina Mwalimu Nyerere alizungumzia sifa za uchumi tegemezi na mgawanyiko kati ya nchi tajiri za Kaskazini na nchi maskini za Kusini. Mwalimu akasisitiza kwamba mgawanyiko huo hauwezi kuendelea katika dunia hii moja kwa sababu watu wa Kusini hawawezi kuendelea kuvumilia. Hali hii ni hatari kwa amani ya dunia. Alisisitiza kwamba huwezi ukawa na amani bila haki. Baada ya hoja hizi, Mwalimu akageukia hali ya ndani, akifananisha mgawanyiko wa matajiri na maskini nchini na mgawanyiko kati ya nchi tajiri za Kaskazini na nchi maskini za Kusini. Katika muktadha huu ndipo, kwa mara ya kwanza, Mwalimu mwenyewe alifanya uchambuzi wa Azimio la Arusha na nafasi yake kisiasa nchini. Endelea kusoma .... ....]*

Sasa baada ya kusema hivyo, nasema nianze kusema ule mgawanyiko wa nje na ndani. Mgawanyiko kati ya Kaskazini na Kusini, unaoleta unyonge, unawezekana pia ndani; katika nchi yetu nako tunaweza. Sasa hivi nasema. Ngoja nitumie kofia yangu ya tume ya ushirikiano nizungumze, lakini nizungumze mambo yale yale.

Kaskazini na Kusini naona sana ni mgawanyiko kati ya kaskazini inayotawala na kusini inayotawaliwa. Nasema lazima tusaidiane kwa sababu tunaishi katika

dunia moja. Wote ni binadamu; sehemu ndogo iliyoendelea ya Kaskazini iendelee kututawala wengi tulio Kusini kana kwamba si watu sisi. Hii hatuwezi kuikubali hata kidogo.

Ujumbe huu lazima uende Kaskazini kutoka Kusini. Haiwezekani tuishi katika dunia moja halafu tukakubali. Kule kutawaliwa kwa nguvu shauri nyingine, lakini kukubali ni aibu. Mnatukana Mungu. Mnakubali unyonge. Kwa nini? Kwa hiyo lazima kutuma ujumbe huo. Sasa naivua kofia yangu naiweka.

Sasa ndani ya Tanzania: kwamba mgawaniko kati ya Kaskazini na Kusini inaweza kuwa nchi. Kwa hiyo, kutakuwa Kaskazini kugawa Kusini katika Tanzania. Tutakuwa na watu Tanzania wanaishi maisha ya Kaskazini tu kana kwamba hawako Kusini. Hii si kweli, haiwezekani… Walio wengi hawawezi kukubali hata kidogo. Hawatakubali, walio wengi hawa miaka 11 kufika karne ya 21; hawawezi kukubali mgawanyiko huo.

Kwa hiyo, mnaweza hata ndani ya Tanzania kuwa na kikundi cha watu wachache kinachotawala uwezo wa uchumi na kwa hiyo kutawala uwezo wa kisiasa. Na wale walio wengi ambao ukiwauliza wanasema sisi tuna uchumi tegemezi, hapa ndio wote wataitwa wa '*informal sector'*. Eh! Idi anasema wengi nchini Peru. Nilikuwa nchini Peru, sasa wanakuwa ni watu wa aina hiyo wengi wao. Tunaweza kuwa na mgawanyiko huo pia hapa. Sasa mimi kwa kofia yangu ya pili, wenzangu, nasema hilo hatuwezi kulikubali wote hapa katika itikadi yoyote.

Tunakubali hiki kitu tunachopambana nacho kimataifa tukionee haya kupambana nacho ndani, ambako tuna uwezo? Kwa sababu ulimwenguni uwezo wetu ni mdogo; ndani tuna uwezo.

Kwamba tutakuwa wanafiki tu, tunawaambia wa Kaskazini kwamba mgawanyiko haukubaliki wakati huo huo nchini Tanzania sisi - sisi tunajenga mgawanyiko huo, na tunadhani tunakuwa waaminifu mbele ya nani? Si mbele yetu wenyewe, si mbele ya Mungu, si mbele ya nani. Tutakuwa waaminifu

mbele ya nani kama tutafanya hivyo?
Sasa wenzangu mmesimama hapa. Patel kasimama hapa akasema vizuri kabisa: 'Tunashukuru kwa ushirikiano mzuri kwa Watanzania.' Hapa amani nzuri hakuna utengano wa ukabila au nini! Yote kasema sawa, ni kweli. Mengi alisema vilevile, tuko hapa, tusingekuwa hapa bila msimamo wa Chama – tusingekuwa hapa. Sawa sawa, tuna utulivu safi kabisa, hii ni kweli kabisa; kitu chetu cha kujivunia kikubwa kabisa ni hicho tu – tuna utulivu wa hali ya juu katika nchi hii. Eh! Mwakitwange alirudia katika mada yake kusifu utulivu.

Lakini Waswahili wanasema ukiona vyaelea vimeundwa. Vimeundwa. Sio tu utulivu umekuja wenyewe tu. Utulivu wa Tanzania sio kwamba Azimio la Arusha limeondoa umaskini hata kidogo. Umaskini si huu bado tunaendelea nao? Si huu mpaka leo? Uchumi si huu huu bado tunasumbuka nao? Si kwamba Azimio la Arusha limeondoa umaskini hata kidogo, wala halikutoa ahadi hiyo. Azimio la Arusha limetoa ahadi ya matumaini. Ya haki, ahadi ya matumaini kwa wengi, ndio watu wengi wa Tanzania wanaendelea na kuwa na matumaini hayo. Madhali yapo matumaini hayo, mtaendelea kuwa na amani. Hapa tuna umaskini Tanzania, lakini hakuna '*social cancer'*. Inawezekana, sijui kama kameanza anza kidogo, sijui; lakini hatuna '*social cancer'*. Hakuna '*volcano'* inayojengeka kwamba ukiweka sikio chini hivi, unasikia hiyo '*volcano'* inajengeka na kwamba siku moja italipuka tu. Hatujafika hapo bado kwa sababu watu bado wana matumaini yanayotokana na msimamo wa Azimio la Arusha. Halikuondoa umaskini lakini limewapeni wote nyinyi wa chumba hiki, mabepari na wajamaa, limewapeni nafasi hiyo – kwamba mjenge nchi ina matumaini kwa wengi. Bila hivyo hamna, watakataa; na mtawafanyaje?

Hivi kweli mtawafanyaje? Hivi kweli Waswahili wachache nyinyi mtawale Watanzania kwa nguvu bila matumaini, halafu watakaa tu kwa amani – amani ya matumaini – matumaini yakiisha kutakuwa na ghasia za kijamii na nitawashangaa Watanzania hawa wakatae kufanya ghasia. Kwa nini?

Hivi sasa katika kofia yangu ile nawaambia Wazungu wa Kaskazini. Nasema hivi, msingi wa amani duniani ni haki. Kwa hiyo, kama mnataka amani ya kweli sio kwamba mashariki na magharibi mzungumze yaishe, hata kidogo. Kwa hiyo, mtakuwa mnaondoa migogoro yenu mtaona mmetengeneza namna moja ya haki, lakini bila kuondoa migogoro ya Kaskazini na Kusini, amani tutaikataa sisi. Haitakuwa dunia ya amani kwa sababu ni watu sisi na ndani ya kila nchi ni hivyo hivyo. Uingereza ni hivyo hivyo, Marekani ni hivyo hivyo, Ujerumani ni hivyo hivyo na Tanzania ni hivyo hivyo.

Kama wengi hawana matumaini, tunajenga '*volcano*'. Siku moja italipuka na lazima ilipuke. Isipokuwa watu hao wajinga. Wengi wa nchi hiyo wajinga, wanakubali kutawaliwa hivi hivi. Kuonewa hivi hivi na wingi wanao, wajinga hao. Kwa hiyo, Watanzania hawa watakuwa wajinga, wapumbavu, kama wataendelea kukubali kuonewa na watu wachache katika nchi yao. Kwa nini?

Kwa hiyo hatuwezi tukasema sasa eti umefikia wakati tukasema Azimio la Arusha tulisahau. Msijidanganye hivyo. Hiyo ni sawa na mjinga ametumia ngazi amepanda amefika juu, halafu anaipiga teke ile ngazi. Unaipiga teke ile ngazi, haya kaa huko maana tutakata jiti sasa. Sisi tuko chini, wewe uko juu; ngazi umekwishaipiga teke, tutaliangusha sasa jiti – nalo ni refu hili. Kishindo chako cha kuanguka bwana kitakuwa kikubwa kweli, tusiseme hivyo.

Sasa nasema hiyo nayo inatosha, baada ya kusema hapo inatosha; lazima tukubali msingi wetu, msingi wetu wa kujenga hiyo amani tuendelee na imani tuendelee. Wananchi wa Tanzania waendelee kuamini Chama, kuamini serikali, kuamini nyinyi wenye nafasi – wawaone nyinyi ni wenzao, wasiwaone nyinyi ni maadui zao. Waamini Chama, waamini serikali – nyinyi mliopata nafasi maana hakuna nchi watu wote sawa. Hata vidole vyangu hivi si sawa, hakuna usawa wa namna hiyo.

Lakini waamini serikali. Wakiamini Chama chao, wawaamini nyinyi mliotangulia mbele wawaone kwamba kwa kweli wote pamoja, kwamba mmetangulia lakini shabaha yetu ni ile ile: kujenga nchi ya haki. Hapo

tukikubali msingi huo sasa nasema tushindane. Tushindane katika hali hiyo tunaendelea kujenga sekta ya umma. Kwa nguvu. Tunaipunguzia udhaifu wake; zingine za ovyo ovyo, zingine za kijinga-jinga. Tunazipunguza kujenga sekta ya umma, hata kidogo, msije mkadanganyika hata kidogo.

Tutazidi kuongeza sekta ya umma na kuifanya imara. Sio dhaifu hata kidogo. Lakini sekta ya binafsi ipo tangu 1967 na kabla, sasa fanyeni kazi nzuri lakini tukabiliane na watu wa nje kwa pamoja. Mtu ambaye tutamkataa sisi ni yule ambaye kazi yake yeye ni kutufanya sisi tu ni wafanyakazi wa nchi za Kaskazini. Huyo si mwenzetu hata kidogo. Si mwenzetu, Mengi. Jifanye bepari mzalendo, tutakuunga mkono asilimia mia moja kama bepari mzalendo. Hatutakusaidia, tutapambana nawe kama utajaribu kuifanya nchi hii koloni mamboleo kwa ajili ya mtu mwingine nje ya Tanzania. Tuelewane hivyo. Kuwa bepari, tengeneza fedha, lakini fedha hizo kwa ajili ya Tanzania – kwa ajili ya kujitegemea kwa nchi yetu – lakini tukupe uwanja wa nchi yetu uutumie kutufanya wafanyakazi wa watu wengine, hatukubali hata kidogo. Tutapambana na nyinyi mkiwa namna hiyo. Ndio maana sasa hivi tunasema waziwazi. Tujenge nchi yetu. Hatutaji, katika hali ya kujaribu kuutoa uchumi wetu katika hali hii ya ovyo, tutatumia uwezo wetu wa ndani kwa ajili ya maendeleo, ubepari na ujamaa. Tutazichanganya zote hizi kwa nguvu kabisa kabisa kujenga uchumi wa nchi yetu.

Lakini hatutajifanya kwamba eti tukisahau msingi wa Azimio la Arusha tutaendelea kubaki na amani katika nchi. Uwongo, haiwezekani. Kwa hiyo, lazima tukubali kushirikiana hivyo kwa msingi huo.

Sasa, mwisho kabisa nitasema haraka haraka. Jamani nyie katika jitihada hizi za kuanza kujitegemea kidogo, mambo machache yafuatayo tukubaliane tuyafanye. Kwanza, lazima tujitegemee kwa chakula. Lazima tuseme kwamba tutaacha kuombaomba chakula. Sasa nchi inajitegemea kwa chakula… sijui Patel zile eka zako 12,000 unalima nini? Pilipili? Lazima tujitegemee kwa chakula. Hilo liko katika uwezo wetu. Kusema kwamba Watanzania hawawezi kujitegemea kwa chakula ni uongo. Tunaweza kujitegemea kwa chakula.

Sasa tufanye hivyo basi, maana aibu sana watu wazima kuomba chakula kila siku. Na matajiri hawa hawana haya. Waswahili tunaona haya kumsimulia mtu kitu kama chakula. Kumsimulia mtu kwa chakula ni kumsemasema. Unampa chakula halafu unamsema kwamba watu hawa bwana kwao hawali. Akija kwako hapo atakaa wee haondoki, na anasikia hivyo. Sasa waswahili hawapendi tabia hiyo. Mtu unaweza kumsimulia kitu kingine chochote lakini chakula; chakula hasimuliwi mtu bwana. Lakini wenzetu hawa wakubwa, anakupa chakula huku anakusema bwana. Anakupa chakula kwanza halafu wakati uleule wanatuwekea vikwazo sisi tusijitegemee katika jambo la kilimo. Wao wanatoa ruzuku kwa kilimo chao, wana mapesa mengi kwa hiyo vilimo vyao ni vyenye ufanisi kabisa.

Kilimo cha Wamarekani hakiwezi kushindana wakiondoa ruzuku. Waondoe; kama hodari kiasi hicho si waondoe ruzuku! Maana sisi wametuambia tuondoe ruzuku, tumeondoa. Ndugu Rais, na wao waondoe basi maana wanajidai hodari sana hawa. Waondoe, waache kuwapa wakulima wao pesa za bure. Wakulima wao na wakulima wa Kusini tushindane tu; kama wanatuweza, waondoe kesho. Si wanajidai hodari sana. Sitaki kusema zaidi, nasema ingawa kilimo jamani, ndugu Rais, tujilishe wote hawa tunaolima, tujilishe. Hilo la kwanza, tujilishe kwa chakula; sisi tunaingia karne ya 21 bado hatujilishi kwa chakula. Majitu mazima, tumesomesha watu wengi sana, wasomi tele. Pili, mavazi. Tulipofanya rasilimali zile kubwa katika viwanda tukasema tunalima pamba sisi. Sasa tunalima pamba, halafu pamba yetu tunauza nje. Watu wazima tunalima pamba, tunauza nje; sasa angalau tuanze kutengeneza nguo. Kwa hiyo, lengo letu la mwanzo, tulikuwa tunataka – tulitaka kutumia pamba yetu asilimia 60 ndani na asilimia 40 kuuza nje. Sasa sijui tunauza kiasi gani… Tunatumia theluthi moja, kama asilimia 30. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile hatujafikia, lakini rasilimali inatosheleza. Kwamba kama viwanda hivi vingekuwa vikitumika kwa uwezo wao wote, pengine vingesogelea hapo au hata kuvuka viwanda tulivyonavyo. Sasa ninasema katika hilo uwezo tunao. Ingawa bado uwezo wa kutengeneza viwanda vyetu wenyewe hatuna, lakini viwanda hivyo tulivyonavyo tuvitumie basi angalau tujitosheleze kwa nguo – kwa mavazi – kwa maana ya mavazi, yaani nguo zenyewe na viatu. Sisi

tuna ng'ombe, tuna mbuzi; tunaendelea, watu wazima tunauza ngozi nje, ngozi hasa… tufanye hivyo, maana uwezo tunao, sio wa kutafuta, rasilimali ipo tayari… Mengi, hilo tunaweza tukafanya.

Tatu, madawa, madawa… Madawa hili nalo tunaliweza bwana, hivi kweli au hata vidawa vya hospitali zetu. Ndugu Rais, kitu cha kutengeneza dawa za hospitali, maana dawa za hospitali miaka 11 kabla ya karne ya 21 bado hatuwezi kufanya hivyo? Hivi hatuwezi kuwa na orodha maana tulitengeneza ya madawa muhimu. Nasema madawa haya kwetu sisi ndiyo ya lazima. Hatuwezi kuyatengeneza?... Tuzitengeneze sisi wenyewe hapa, tuna viwanda viwili sisi hapa. Nadhani tuna viwanda viwili au vitatu sijui vya kutengeneza dawa. Na vitengeneze ama vigawane kazi; kimoja kitengeneze dawa hizi, hiki kitengeneze dawa hizi, hiki kitengeneze dawa hizi na kile tusichokiweza tukitafutie uwezo, tutengeneze dawa zile za lazima.

Tunayo orodha ya madawa muhimu, tunaweza kutengeneza. Kwa nini kwa afya ya watu wetu vilevile tuwe tegemezi? Hata afya ya watu tunakuwa tegemezi. Vitu vidogo sana kuweza kutengeneza dawa na tunaweza kutengeneza dawa. Najua wakubwa hawapendi. Brazil wanatengeneza dawa, wamebanwa na Marekani; nimeambiwa kwamba ingawa wanatengeneza dawa karibu kujitosheleza, hii sekta ya nyumbani ya dawa hii sehemu kubwa kabisa ni ya Marekani. Lakini hata hivyo, wamebanwa na wakubwa.

Sasa dawa angalau tutengeneze. Tujitegemee katika kitu kama dawa sio kwa kila kitu lakini kwa madawa ya lazima. Tuna matatizo ya afya. Sasa hilo nalo tuendelee kuwa tegemezi? Tunauziwa unga lakini miaka 11 kutoka karne ya 21 wanatuuzia vidonge vya unga wa muhogo, sijui. Tunalisha watu wetu, wataalam, nyinyi hamuwezi kutukomboa kwa hilo?

Vifaa vya elimu… vifaa vya elimu. Mengi, si ulianza na kalamu? Sasa tuanze, tutengeneze karatasi. Leo tunatengeneza vifaa vya elimu vinatupa taabu tuna watoto wengi wanaosoma. Tuna watoto wanasoma kama milioni nne. Mimi nadhani kusema kweli tunaweza tukawa na viwanda maalum tu kwa shughuli

za vifaa vya elimu. Tunaposema kwamba tunataka watoto wa shule wavae viatu, tunajua viatu vyenyewe vinapatikana wapi? Eh! hivi viatu tu, kusema viatu, sijui watu wana viwanda vyao wenyewe, sijui maduka yao wenyewe? Angalao tuseme, kwa shughuli za shule, tunatengeneza. Hivi yunifomu zinatengenezwa mahali fulani, hizi kalamu madaftari yanatengenezwa mahali fulani. Tufanye hivyo, maana kubwa jambo hili, ni kubwa kwetu; kusomesha watu wetu ni kubwa, na uwezo tunao, sio kwamba hilo nalo tena ni kazi ya kuweza kutegemea Kaskazini. Hivi sasa ni balaa kupata madaftari katika shule zetu. Watoto hawana daftari, walimu hawana ile chaki ya kuandika.

Mwisho. Nimeyasema hayo: chakula, mavazi, madawa ya watu na mifugo, vifaa vya elimu, na spea mbalimbali. Yule Mhindi aliyekuwa akiniambia bomba ni za spea. Leo Tanzania mtu wa nchi anaweza akatupa gari lake bure bure, akasema hilo gari chukua bure madhali utanunua spea kwake. Kwa hiyo, matumizi yetu ya spea hapa ndiyo huyu Mhindi alikuwa akisema bomba, lile bomba… lile bomba hasa linazoa fedha zinazokwenda nje bure. Kama lazima, sawa. Kile kitu ambacho hukitengenezi na huna uwezo wa kukitengeneza na unataka agiza kutoka nje.

Lakini spea nyingi ni bure, za magari yetu, za matrekta. Hayo tungetengeneza. Ndugu Rais, nimechukua muda wenu mrefu sana na (….) matatizo. Niwashukuruni sana.

(Chanzo: Gazeti la *Mzalendo*: Jumapili Mei 21, 1989)

# Sura ya Nne

# Kila Zama na Kitabu Chake

*Ali Hassan Mwinyi*

## Maamuzi ya Zanzibar, 1991

*(Hotuba ya Mwenyekiti wa CCM, Rais Ali Hassan Mwinyi wakati akizungumza na wazee wa chama, viongozi wa taifa, mashirika ya umma na watu binafsi juu ya ufafanuzi wa maamuzi ya Halmashauri Kuu ya Taifa katika kikao chake cha Zanzibar: Diamond Jubilee Dar es Salaam, tarehe 25/2/1991)*

Ndugu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Mkoa wa Dar es Salaam,
Ndugu Katibu Mkuu,
Ndugu Mwenyekiti wa Wazee wa Dar es Salaam,
Ndugu Viongozi wa Chama na Serikali na
Ndugu zetu waalikwa,

Kabla ya yote, labda niseme kwamba kwa kuwa tumo katika mwezi wa pili tokea kuanza kwa mwaka mpya, nami sijapata nafasi ya kukutana nanyi wazee, ni vyema nitumie nafasi hii kwanza kukutakieni heri ya mwaka mpya, na baraka zote za mwaka 1991. (Makofi). Ninakuombeeni uzima, nguvu, baraka na mafanikio.

Pili, tuna kawaida katika nchi yetu, kwamba kila linapotokea jambo muhimu katika Taifa, tunatafuta nafasi ya kukutana nanyi na kukuelezeni. Hivyo, leo napenda kuzungumza nanyi wazee wa Dar es Salaam na, kupitia kwenu, iwe ninazungumza na Wazee wenzenu wa Tanzania nzima. Kwa hiyo, hayo nitakayokuambieni nyinyi, ninawaambia pia Wazee wa Taifa letu wote kwa jumla.

Hivi karibuni Halmashauri Kuu ya Taifa ilifanya kikao chake cha kawaida Zanzibar, ambacho kilijadili mambo mbalimbali. Kikao hicho kilimalizika kwa kutoa maamuzi maalum. Maamuzi hayo yana uzito mkubwa. Inaelekea baadhi yetu, pamoja na Vyombo vyetu vya Habari, hatukuyaelewa vizuri maamuzi hayo. Kwanza, nataka nivivue lawama Vyombo vyetu vya Habari. Maana hatukuwa nao huko. Kwa hivyo walitangaza vile walivyoelewa. Kwa sababu hiyo nimeona ni vyema kuzungumza nanyi ili kusahihisha matangazo ya vyombo vyetu. Nimeona ni vyema kutumia nafasi hii kutoa ufafanuzi.

## Lazima Twende na Wakati

Inaelekea kuna hofu kwamba Azimio la Arusha linageuzwa. Kwa hiyo, tokea mwanzo, kabla ya kusema lolote, nataka tuelewane kwamba siasa yetu bado ni ile ile ya Ujamaa na Kujitegemea. *(Makofi)*. Haikugeuka wala hatutazamii kuigeuza. Kwa hali yoyote sisi Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi hatutaigeuza Siasa hii. *(Makofi)*. Kule Zanzibar tulizungumza mambo mengi, miongoni mwao, ni kutoa tafsiri ya baadhi ya vipengele vya Azimio ili vifanane na wakati tulionao.

Azimio la Arusha, kama tunavyojua, limetangazwa mwaka 1967. Hii leo tuko katika mwaka 1991. Imepita miaka mingi, zaidi ya 20 tokea kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Na katika kipindi cha miaka 20 yametokea mabadiliko mengi duniani na pia katika hali ya maisha yetu. Hali yetu ya sasa, hasa ya kiuchumi, siyo ile ile ya mwaka 1967. Ndio maana mishahara ya wafanyakazi ingawa imeongezeka sana lakini bado haikidhi mahitaji yao - haiwatoshi hata wale wanaopokea mishahara mikubwa miongoni mwetu. Isitoshe, wakati wa Azimio idadi ya Watanzania ilikuwa ndogo. Sasa hivi idadi yetu imeongezeka zaidi ya mara mbili. Kwa sababu ya wingi wetu mahitaji yetu nayo yemeongezeka sana, wakati mapato yetu yamekuwa yakipungua wakati wote.

Kwa hivyo ni dhahiri kwamba jamii ya Tanzania lazima itie maanani mabadiliko haya na ijiandae kwenda na wakati. Kama hatukwenda na wakati, kazi yetu itakuwa ni kufukuzia wakati - jambo ambalo hatulimudu.

Tabia ya wakati ni kama ile ya bahari. Bahari inakupwa na kujaa mpaka ukingoni mwa maji. Baadaye maji huopwa polepole, mpaka kufika wakati ikawa maji yote yamekwishaondoka ufukoni. Samaki werevu huondoka nayo hayo maji, yaani yakijaa huja nayo, yakitoka hutoka nayo, vinginevyo hupwelewa. Samaki watakaozembea kufuata maji watajikuta wamechelewa wanatapatapa juu ya mchanga wakati maji hayo hayapo. Hiyo ndiyo maana ya kupwelewa *(Makofi)*.

Hapa Afrika, kwa mfano, imeanzishwa mipango mbalimbali ya ushirikiano wa uchumi. Mipango hiyo ni pamoja na Ushirikiano wa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADCC) na Eneo la Soko Nafuu (PTA). Afrika pia imeazimia kuunda Jumuiya ya Uchumi. Nchi zinazoendelea nazo zimedhamiria kuzidisha ushirikiano miongoni mwao. Nchi yetu lazima ifanye mabadiliko ili iweze kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli zote hizo zinazosaidia maendeleo yetu.

## Kila Zama na Mwongozo Wake

Ndugu Wazee, Msahafu wa Waislam unasema "LIKULLI AJALIN KITABU" Mwingereza mmoja kaitafsiri aya hiyo hivi: "TO EVERY AGE ITS BOOK" yaani "Kila zama ina Kitabu (Mwongozo) chake". Na sisi Wana-CCM tunakubali kuwa "kila Zama zinahitaji kuwa na Mwongozo wake". Azimio la Arusha ni Mwongozo wetu wa msingi. Ni dira inayoongoza mwelekeo wa jamii yetu. Lakini tafsiri zake zinabidi zirekebishwe kila inapohitajika ili zisipitwe na wakati. Miongozo ina tabia moja: inakuja ili kufafanua, kuelekeza au kukemea hali mbaya inayojitokeza.

Mojawapo ya malengo ya maamuzi ya Zanzibar ni kutoa tafsiri sahihi ili kupunguza kebehi inayofanywa dhidi ya siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea na pia kwenda na wakati.

Mwaka 1967 lilitangazwa Azimio la Arusha. Mwaka 1971 ulifuatiwa na tamko la Iringa la "Siasa ni Kilimo". Tamko hili lilikuwa ni mbinu na msisitizo wa Siasa yetu ya Kujitegemea. Lilipanua tafsiri ya Azimio la Arusha. Katika mwaka 1981 ilionekana kuna haja ya kutolewa mwongozo

mwingine kulingana na wakati ule ambao nao ni upanuzi wa tafsiri ya Azimio. Ulitangazwa ili kukidhi haja ya wakati ule.

Aidha, kabla ya hapo, katika mwaka 1974, Chama kilipitisha Agizo la Musoma kuhusu Elimu ya Kujitegemea ambalo madhumuni yake yalikuwa kutazama upya suala la uingizaji wanafunzi Chuo Kikuu na kupanua Elimu ya Msingi ili kutoa fursa kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule kufanya hivyo.

Maandiko yote hayo hayakupingana na Azimio la Arusha ila yakiongeza mwangaza kwa mambo ambayo yalihitaji yafanane na wakati wake. Na lazima iwe hivyo, kwani bila ya kwenda na wakati tungechekesha.
Kwa mfano wakati wa Azimio la Arusha, mtakumbuka kuwa tafsiri ya neno Kiongozi ni pamoja na yule mwenye mshahra uliofikia shilingi 1,066/= kwa mwezi. Tungeng'ang'ania tafsiri hii tu, basi leo pasingekuwapo wafuasi. Wafanyakazi wote wangetafsirika kuwa ni viongozi wa CCM. Kwani ukiacha wakulima, wafanyakazi wote sasa kwa tafasiri ya 1987 ni viongozi tena maradufu. Maana kima cha chini sasa ni Sh.2,500/=, ambazo ni zaidi ya mara mbili ya Sh.1,066/=. Ndiyo maana tukasema jamii yetu italazimika kufanya marekebisho kila inapokuwa lazima kufuatana na wakati. Tutafanya hivyo bila ya kuachana na misingi ya siasa yetu.

Kwa hivyo, tulichokifanya kule Zanzibar ni kupanua tafsiri za Azimio ili ilingane na wakati tulionao. Kufanya hivyo si kuua Azimio bali ni kuliimarisha.

### Chimbuko la Azimio la Arusha

Historia ya Azimio la Arusha tunaijua sote. TANU ilipigania kwa maneno mpaka nchi ikapata UHURU wake. Tanganyika ilipopata Uhuru na tukaanza kujitawala ishara potofu zilianza kuchomoza. Baadhi ya viongozi walianza kuutumia uongozi wao kama mradi wa kujineemesha. Kwa kutumia nyadhifa zao, wakikopa fedha benki na kuanza kujijengea mashamba - si ya miti - bali ya majumba; si nyumba za kuishi tu bali majumba mengi ya kupangisha.

Tabia hiyo ilizusha manung'uniko ya watu. Jamii ilianza kugawanyika makundi mawili; manaizi na makabwela. Kitendo hicho ndio chimbuko la

kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Azimio lilikuja kutoa mwongozo wa maadili ya wanachama na viongozi wa TANU. Kwa hivyo nia ya Azimio la Arusha, miongoni mwa mambo mengine, ilikuwa ni kuwazuia viongozi kutumia uongozi wao kujitajirisha. Hilo ndilo lililokuwa tatizo la hatari miongoni mwa matatizo wakati ule. Azimio lilikuja kuokoa jahazi - kukemea tabia potofu.

## Tatizo la Sasa ni Uchumi Tegemezi

Mtu anaweza kuuliza je sasa kuna tatizo gani? Tatizo letu katika miaka ya tisini na kuendelea ni lile la uchumi tegemezi. Tatizo letu sasa ni kwamba uchumi wetu ni duni mno. Wakati idadi yetu inaongezeka, mapato ya Taifa, hasa ya fedha za kigeni, hayaongezeki. Wakati wa Uhuru idadi yetu ilikuwa ni watu milioni tisa. Lakini leo, tuko milioni tisa na tisa tena na nusu ya tisa. Lakini mapato yetu ya pesa za kigeni yapo pale pale, $ milioni 400. Wakati Azimio la Arusha lilitutaka tujitegemee, hali halisi ni kuwa tumekuwa wategemezi wakubwa. Maana Taifa letu hivi sasa, kwa pato lake lenyewe la fedha za ndani, linaweza kujitegemea kwa kipindi cha miezi saba tu katika mwaka. Tunategemea watu wengine, kwa njia ya ruzuku na mikopo, kumalizia miezi mitano inayosalia katika mwaka. Hii ni hatari. Lazima tuendelee kubuni mbinu za kuondokana na hali hiyo.

## Mbinu za Kujitegemea

Ilani ya Uchaguzi inasema hivi:

> Makusudi ya Chama katika kipindi cha miaka mitano ijayo ni kwa Taifa kukusanya nguvu zote za wananchi kwa kusaidiana na Serikali zao (Mbili), na kuzitumia katika kila eneo la maendeleo ili kutoa msukumo mpya wa utekelezaji wa siasa ya Ujamaa na Kujitegmea.

Hivyo, Chama na Serikali zake zinawajibika kuwarahisishia wananchi wao kujitegemea kwa chakula, kujitegemea kwa mavazi na kujitegemea kwa malazi. Ili kutimiza lengo hilo Taifa lazima liwawezeshe wananchi wake kuzalisha mazao ya biashara na chakula kwa wingi. Pia ni wajibu wa Chama na Serikali kuandaa mbinu za kuwasaidia wananchi kujijengea nyumba zao

za kuishi ili ziwasitiri wanapostaafu au kuwa wazee.

Je wananchi wakituuliza: hivi ni mbinu gani mlizofanya kumshirikisha kila mmoja wetu kutumia nguvu zake zote katika kuzalisha kama Ilani inavyosema? Tungejibu nini? Lakini sasa kila mwananchi, pamoja na mwana CCM, hataweza kutoa kisingizio kwa kusema:-

> Mimi sikuweza kutumia nguvu zangu zote katika kufanya kazi ya kuzalisha kwa sababu nimezuiwa na Azimio la Arusha.

## Mwanachama Kuchangia Uchumi Kikamilifu

Azimio la Arusha lipo. Narudia tena kusema kuwa wanaohusika na tafsiri hii ni wanachama. Sisemi Viongozi, bali wanachama wa CCM. Tunataka kumpa Mwanchama wa CCM, kama mwanachama mwingine yeyote, uhuru zaidi wa kuzalisha ili kuchangia kadiri ya uwezo wake katika pato lake yeye mwenyewe na pato la Taifa kwa jumla.

Ili tujitoe, kitaifa, kwenye shimo la utegemezi tulimo hivi sasa, mbinu bora ni kutoa uhuru kwa kila mwananchi wa kila Kaya, wa kila Kata, wa kila Tarafa, wa kila Wilaya na wa kila Mkoa kutumia nguvu zake zote katika kuzalisha. Matokeo ya hatua hii ni kumwezesha kila mtu katika Kaya, Kata, Tarafa, Wilaya na Mkoa kujitegemea. Tukifika hapo ndipo Taifa litapokuwa limeondokana na hali ya sasa ya uchumi tegemezi.

## Kupangisha Nyumba

Jambo la kupangisha nyumba nalitaja tu, kwani si lazima kwa sababu si jipya; hata hivyo ni vyema nalo litajwe. Mwenyekiti Mstaafu alilisemea jambo hili mahali pengi sana, tena alianza zamani kulisemea, sijui. Kwa mfano, hivi karibuni alilitaja tena katika hotuba yake ya kuadhimisha miaka ishirini ya Azimio aliposema hivi:

> Masharti hayo yanamkataza kiongozi wetu kuishi kikabaila kwa mbinu za kupangisha **majumba.**
>
> Lakini sharti hili halimkatazi mtu mwenye vyumba vya ziada katika nyumba yake anamoishi kuvipangisha kwa

watu wengine kwa kodi nafuu, Hili ni jambo la kawaida kabisa katika nyumba zetu za "Waswahili"' na upangishaji huu mimi **nimekuwa nikiutetea tangu zamani.** Utaratibu huu unawasaidia sana watu wenye mapato madogo, wanafunzi, au wafanyakazi ambao bado hawajaoa au kuolewa kupata vyumba vya kupanga kwa kodi nafuu.

**Ni kweli kwamba huko nyuma tumekuwa wakali mno** katika kutafsiri msharti haya.

Azimio la Arusha linachokataa ni unyonyaji. Hivyo maskini ya Mungu mwenye kijumba chake cha mbavu za mbwa akimwona maskini mwenziwe anapata taabu, hana pakukaa, asimpangishe? Je akimpangisha atakuwa anamnyonya? Au anamstiri? Kwa hiyo tangu zamani kustiriana ni ruhusa *(Makofi)*.

Hatukuishia hapo kule Zanzibar, tulikwenda zaidi, tulisema pia kwamba wapo viongozi miongoni mwetu ambao baadhi yao wamefanya kazi za Chama au za Serikali kwa miaka 30 au zaidi. Lakini hawana nyumba; ukifika wakati wao wa kustaafu viongozi hao huwa wanababaika kwa kutojua wataishi wapi. Ndipo wanapoanza kutafuta mbinu - ndiyo maana siku hizi utakuta misururu mirefu katika Ofisi ya Vyeti vya kuzaliwa. Watu wanakwenda kubadilisha tarehe zao za kuzaliwa, kujifanya bado wangali vijana ili wachelewe kustaafu. *(Makofi)*.

Sisi tunaamini kwamba baada ya kipindi kirefu cha utumishi, mtu aweze kuwa na nyumba ili, hata akiwa kipofu angalau aweze kupapasa kuta zake na kusema: Hii ni nyumba yangu niliyoipata kwa jasho langu la kazi ya miaka 30. Tunataka awe na kitu. Lakini, Ndugu Wazee, bahati nzuri wanachama wa CCM, kama wananchi wengine, wanaruhusiwa kukopa. Wanaweza kukopa kwenye benki zetu wakajenga nyumba za kukaa. Sasa jamani tukisema kwamba hata mtu aliyekopa asiipangishe nyumba hiyo atalipia nini huo mkopo?

Vinginevyo tutakuwa tunamfanyia mzaha mtu huyo. Maana atachukua mkopo, ajenge nyumba, kisha ashindwe kulipa huo mkopo. Waliomkopesha wataikamata hiyo nyumba na kuiuza ili kurudisha fedha yao. Katika hali hiyo mwana-CCM gani atakayekuwa na nyumba iwapo mwisho wake ni kuchukuliwa na kile chombo kilichomkopesha? Kwa hivyo nasema mtu kama huyu ana dharura; ana dharura ya deni. Amejenga nyumba kwa nia ya kukaa mwenyewe lakini ana deni la mkopo. Kama anaweza kukaa nyumbani mwake, akae. Lakini pia awe na ruhusa ya kupangisha nyumba yake, akitaka, ili imsaidie kulipa mkopo. Anapostaafu awe anayo nyumba ya kumstiri uzeeni. Kitendo hicho kisimpotezee uanachama wake wa CCM.

Kwa hivyo Ndugu Wanachama, huko ndiko kwenda na wakati, vinginevyo tutapwelewa. Mtu kama huyu aruhusiwe kupangisha nyumba yake, iwe nusu ya nyumba, ama robo ya nyumba au yote *(makofi)*.

## Biashara ya Kupangisha Majumba Bado ni Mwiko

**Lakini kikao cha Zanzibar hakikutengua miiko ya kiongozi wala ya mwanachama wa CCM. Bado ni mwiko kwao kuwa na biashara ya kupangisha majumba.** Kwa mfano, kama kuna mwanachama anayeomba mkopo, akipata anajenga nyumba, halafu anaikodisha, akipata fedha za kodi anajenga nyingine mpya, ambayo nayo anaikodisha na kuendelea kujenga nyingine. Huyo ni mfanyabiashara. Kazi yake ni kujenga na kupangisha majumba. Kikao cha Zanzibar hakikusudii mwanachama wa aina hii. Huyu siye *(Makofi)*.

Vile vile, Mwanachama wa CCM, hata akiwa kiongozi katika mazingira maalum, aruhusiwe kukodisha nyumba yake, ikiwa haihitaji kuikaa wakati ule. Inawezekana haihitaji kuishi katika nyumba yake kwa kuwa kapata uhamisho. Mfano, mtu kahamishiwa Iringa kwa kazi wakati nyumba yake iko Dar es Salaam. Je ikae bure watu waitumie bure tu kweli? *(Makofi)*.

Ni mwanachama wa aina hii ndiyo tulisema huko Zanzibar kuwa aruhusiwe kupangisha nusu ya nyumba ama robo ya nyumba au yote, maadam mtu huyo anapo pengine pa kukaa. Lakini tunasisitiza kuwa bado si ruhusa kwa mwana CCM wala kiongozi wa CCM kuendesha biashara ya kupangisha majumba.

## Hisa katika Makampuni ya Umma, Kupunguza Ukwasi!

La pili lililoamuliwa huko Zanzibar ni kuwaruhusu wanachama wa CCM, kwa kufuatana na hali ya wakati ulivyo, sasa aruhusiwe kuwa na hisa katika kampuni ya Umma. Hii leo tunayo Mashirika ya Umma zaidi ya 400, lakini mengine yao hayana fedha za kuendeshea kazi zao.

Mfano kuna mwananchi mmoja alikwenda kwenye kiwanda cha Umma kutaka huduma ya kusafishiwa ngozi zake. Alipofika hapo alikuta "pamelala paka" ; yaani palikuwa kimya, hapakuwa na kazi yoyote inayofanyika. Kumbe kile kiwanda kilikuwa kimefungwa kwa kukosekana fedha za kukiendeshea ... umeme ulikatwa na wafanyakazi walipewa likizo.

Meneja alimfahamisha huyo mteja kuwa kiwanda kimefungwa kwa sababu ya deni la maji na umeme pamoja na pesa za mishahara ya wafanyakazi. Huyo mteja alikubali kulipa arubuni (advance) ya milioni saba ili kukikwamua kiwanda. Wiki ya pili yake kiwanda kilianza kufanya kazi zake za kuzalisha kama kawaida.

Kisa cha kiwanda hicho kusimama kazi ni kukosa fedha za kuendeshea. Kiswahili cha siku hizi huitwa ukwasi. Kwa hiyo kazi ilisimama.
Katika hali kama hii, **tumeona ni vyema kuwaruhusu wananchi wote pamoja na wakulima, na wafanyakazi wa shirika lenyewe wakiwemo wanachama wa CCM kununua hisa chache kwa kila atakaetaka**

## Ubia wa Umma na Dola katika Shirika

Narudia, watakaoruhusiwa kununua hisa ni wananchi wowote watakaopenda pamoja na wakulima wa pamba, korosho, kahawa, tumbaku na wafanyakazi wa hilo shirika lenyewe. Kwa njia hiyo, Shirika hilo sasa litapata sura mpya, litakuwa ni la ubia kati ya Serikali, wafanyakazi na wananchi. Fedha tunazozizungumzia hivi sasa, za kulipia taa na mahitaji mengine zingetokana na ununuzi wa hisa ili uzalishaji uendelee. Katika hali kama hiyo kiwanda kitakuwa ni mali ya umma kweli. Maana kuna tofauti ya Shirika la Dola na Shirika la Umma kwa maana ya wananchi wenyewe.

Endapo shirika la umma litataka kuwashirikisha wananchi na wafanyakazi wake kwa kulichangia ili kuondoa tatizo la Ukwasi, jambo hilo liwe ni halali, na Mwana CCM naye aruhusiwe kuwa miongoni mwao. *(Makofi)*.. **Kilichofanywa na maamuzi ya Zanzibar ni kumruhusu mwanachama wa CCM naye kushiriki kikamilifu katika sera ya Taifa ya uwekezaji wa rasilimali nchini.**

Katika sera ya uwekezaji rasilimali tunaruhusu ubia katika uchumi wetu. Ubia huo unaweza kuwa baina ya watu wa ndani ya nchi peke yao, au kati ya wawekezaji wa nje na wa ndani. Baada ya kuikubali misingi hiyo hatuoni kwa nini tusianzie kwa kuwaruhusu wananchi, wakulima na wafanyakazi kuwa na hisa katika Mashirika wanayofanyia kazi (Makofi).

## Wafanyakazi Kusimamia Uwajibikaji

Nia nyingine ya kufanya hivyo inatokana na kutambua kuwa wafanyakazi wenye hisa katika kiwanda watakuwa wasimamizi wakereketwa wa uwajibikaji katika viwanda hivyo. Watakereketwa zaidi pakiwa na ubadhirifu au kutowajibika.

Hivi leo baadhi ya mashirika ya Umma ni mashirika ya umma kwa jina tu. Watu wanayaibia wakidai wanachukua chao. Pengine wanashindana kufanya hivyo ili wasipunjwe. Baadhi ya mashirika ya Umma yanahujumiwa kana kwamba hayana wenyewe. Baada ya maamuzi ya Zanzibar kuanza kutekelezwa, Mashirika hayo yatakuwa na wenyewe.

## Mwongozo wa 1981 kuhusu Uwajibikaji

Maamuzi ya Zanzibar si mapya. Mwongozo wa chama wa 1981 umetoa ilani juu ya kupungua kwa uwajibikaji katika Mashirika ya Umma, jambo ambalo hivi sasa tunalitafutia ufumbuzi. Mwongozo wa 1981 unasema hivi:

> Imezuka tabia ya aibu nchini ambayo imekuwa ikiongezeka ya vitendo vya kuharibu na kuvitumia vibaya vyombo muhimu vya kazi na mali ya umma kwa jumla. Magari, matrekta, zana nyingine muhimu za chama, serikali, mashirika ya umma mara nyingi hayadumu

muda mrefu kama ambavyo ingetazamiwa kutokana na matumzi mabaya.

Lakini ikiwa watu pale pale wenyewe wana hisa katika kampuni au shirika - mfano – TANESCO – [au] kuwa Mkurugenzi katika kampuni ya Kibepari. Napenda suala hili lieleweke vizuri ili kujibu fikra zilizojengeka kuwa uamuzi huo umevunja Azimio la Arusha.

Kwanza inafaa tufafanue maana ya Mkurugenzi. Tafsiri ya Mkurugenzi inayojulikana sana ni ile ya mjumbe wa bodi ya wenye hisa katika Kampuni fulani. Kwa hiyo wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi katika Kampuni ya Kibepari huwa ni miongoni mwa wale wenye hisa zao katika kampuni inayohusika. Watu hao huchaguliwa na wenzao wenye hisa kama wa kuongoza shughuli za Kampuni yao kwa faida ya pamoja. Mkurugenzi wa aina hii hawezi kuwa mwanachama wa CCM.

Lakini kuna Mkurugenzi wa aina nyingine ambaye ni tofauti kabisa na Mkurugenzi mwenye mali. Mkurugenzi huyu ni yule ambaye ameajiriwa tu na wenye mali yao, kutokana na sifa zake za utaalam, kuendesha kampuni. Mtu huyu huwa ni mwajiri tu, anayefanya kazi. Huyu ni mtumishi tu kama watumishi wengine, hana chake katika kampuni inayohusika. Anachotegemea ni mshahara wake na marupurupu mengine kama yapo. Huyu ndiye Mkurugenzi anayeruhusiwa kuwa mwanachama wa CCM.

Azimio la Arusha bado liko pale pale kwa wale wakurugenzi wa aina ya kwanza. Wao Azimio linawabana, hawawezi kuwa wanachama wa CCM. Lakini huyu wa aina ya pili aliyeajiriwa tu, akija kuomba uwanachama tunamkubali. **Azimio la Arusha kamwe halijamkataa mfanyakazi mwenziwao kwa "koa" la kutumikia Kampuni ya Kibepari, hivyo ndivyo tulivyoamua Zanzibar**

## Mwana-CCM kuwa na Hisa katika Kampuni ya Kibepari

Jambo jingine ambalo halikueleweka vizuri na linahitaji ufafanuzi ni lile la kumruhusu mwanachama wa CCM kuwa na hisa katika kampuni ya

Kibepari. Hili nalo tumeliruhusu huko Zanzibar, lakini sharti iwe katika mazingira maalum.

Ni vyema kukumbushana kuwa yapo makampuni ya kibepari ambayo tumekuwa nayo hata kabla ya Azimio la Arusha. Kampuni hizo zimekuwa zikikidhi kiasi fulani cha ajira ya Watanzania, pamoja na Wanachama wa CCM.

Ni jambo hili lieleweke vizuri, nitatoa mfano tu wa Kampuni ya mtu binafsi. Mwenye Kampuni ya binafsi anaweza kabisa akaamua kwa hiari yake kuuza baadhi ya hisa **kwa wafanyakazi wake** ili kuwapa motisha ya kazi. Tajiri yeyote akiamua kufanya hivyo, Chama na Serikali vitamwona kuwa amechukua hatua ya kimaendeleo. Kitendo chake hicho ni halali. Kwa sababu itakuwa ameuzimua ubepari kwa kuifanya kampuni yake ni ya ubia kati yake na wananchi aliowaajiri. Kwa kweli kampuni hiyo itakuwa kama chama cha ushirika.

Katika hali hiyo, hata Mwanachama wa CCM anaruhusiwa kupokea/kununua hisa alingane na wafanyakazi wenzie. Ni mazingira maalum ya namna hii tu ndiyo yanayoruhusu Mwanachama wa CCM, kama mfanyakazi mwingine, kuchukua hisa katika Kampuni **anayofanyia kazi.** Atakapostaafu ataweza kuendelea kupokea faida ya hisa yake au kuiuza.

## Mishahara Miwili kwa Mwana-CCM

Kuhusu mishahara miwili, Azimio la Arusha linasema hivi:

> Kwamba kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake.

Kufuatana na ukweli huo, anayefanya kazi mbili za halali anastahiki kupata malipo ya kazi ya pili. Tuchukue mfano wa Profesa ambaye mchana kutwa anasomesha Chuo Kikuu. Baada ya saa za kazi anaweza kuamua kufanya kazi ya akili, kwa mfano kutoa ushauri au kuandika mradi kwa aliyemwomba huduma hiyo.

Mwanachama huyo atastahiki kupata malipo ya kazi hiyo. Hili si geni, katika sherehe za kuadhimisha miaka 20 ya Azimio la Arusha, baba wa taifa alisema hivi:

> Lile sharti la kutopokea mishahara miwili kwa kweli ni sharti la tahadhari tu. Ni vigumu sana kufanya kazi mbili za kuajiriwa na zote mbili ukazifanya vizuri. Huwezi kuwatumikia mabwana wawili! Lakini sharti hili halimkatazi kiongozi wetu kujiongezea pato kwa kutumia muda wake wa kupumzika kwa kufanya shughuli nyingine: kama kulima au kufuga, ikiwa yeye si mkulima au mfugaji, kuandika, kufanya kazi ya useremala, au kufanya shughuli nyingine yoyote kwa mikono yake au kwa ajili zake.

Jambo la msingi ni kwamba lazima twende na wakati. Mwaka 1967 lilipotungwa Azimio la Arusha ilikuwa hakuna haja ya kuwa na mishahra au malipo ya kazi zaidi ya moja kwa sababu wakati ule mshahara mmoja ulikuwa unatosha kukidhi mahitaji yote muhimu. Kwa mfano, mimi, mwenyewe, mshahara wangu wakati ule ulikuwa shilingi 2,200/= kwa mwezi. Mshahara huo, hasa kwa Zanzibar, ulikuwa ukinitosha kukidhi mahitaji yangu yote ya lazima.

Wazee wangu watakumbuka kwamba wakati ule kule kitunguu, pilipili na bizari - vyote hivyo kwa senti tano tu. Ilikuwa inawezekana pia kununua samaki mkubwa kiasi kwa senti ishirini mpaka 50 tu; au kununua kuni za kuweza kupikia mlo mzima kwa senti kumi tu. Siku hizo iliwezekana mnunuzi kujaziwa mafuta ya kupikia au samli kikombe kizima kwa senti ishirini au sitini tu. Halikadhalika kwa senti ishirini tu mtu aliweza kununua matunda, kama vile fungu la ndizi mbivu au machungwa au papai. Kwa ufupi, kwa mahitaji ya siku nzima, tangu asubuhi hadi jioni, iliwezekana mtu kutumia pesa kidogo sana.

Katika hali hiyo, kulikuwa hakuna ulazima wa kufanya kazi ya pili. Afanyae kazi zaidi ya moja huonekana ni mlafi au ana tamaa. Kwa mshahara huo huo niliweza kudunduliza pesa na mwishowe kununua gari mpya kabisa. Gari hilo lilinigharimu pesa nyingi kwa wakati huo - shilingi 13,000/=!! Wakati huo bei ya mafuta nayo ilikuwa shilingi tatu tu kwa galoni zima. Katika mazingira ya aina hii mshahara mmoja ulimudu kukidhi mahitaji ya wafanyakazi wengi ukiacha walevi.

## Hali Imebadilika

Lakini leo mambo yamebadilika. Gharama ya maisha imepanda sana. Serikali yenyewe imeungama waziwazi kuwa haina uwezo wa kumlipa mfanyakazi wake mshahara unaomwezesha kumudu gharama za maisha. Kutokana na hali hiyo, wafanyakazi wengi, wanashindwa kukidhi mahitaji yao muhimu. Ndio maana Chama na Serikali yake vimekuwa vikiwahimiza wafanyakazi kufanya shughuli nyingine za halali, baada ya saa za kazi, ili kujiongezea mapato. Mfano wa kazi hizo ni kama vile: kutibu, kuandika vitabu, kuandika mradi, kutoa ushauri wa kitaalamu, kufundisha, 'overtime', useremala, ufundi bomba, ufundi umeme, ufundi cherahani, kilimo, ufugaji, kuziba mipira ya magari, kuteka maji ya kuuza, kupiga matofali, kutengeneza baiskeli na kadhalika.

## Kofia Mbili Mshahara Mmoja

Lakini lazima tuelewane kuwa hii mishahara miwili tunayozungumzia haimhusu kiongozi mwenye kofia mbili. Kwa mfano, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, ambao vile vile ni Katibu wa Chama wa Mkoa au Wilaya, hawaruhusiwi kupokea mishahara miwili. Hawa watalipwa mshahara mmoja tu, maana hii kazi ya pili ni sehemu tu ya ile ya kwanza. Lakini wanaruhusiwa kufanya kazi za ziada kama vile kilimo, ufugaji na kadhalika, baada ya saa za kazi, kama walivyoruhusiwa wafanyakazi wengine. Hapa nitapenda kusisitiza kuwa wale watu wanaoeneza maneno ya kejeli kuwa ati Maamuzi ya Zanzibar ni mbinu tu za "wakubwa" kujifufanisha wenyewe, ijulikane kuwa si kweli. Kazi zilizoorodheshwa hapa si za wakubwa bali ni kazi zinazoweza kufanywa na kila mtu kufuatana na ujuzi alionao na mazingira ya mahali anapofanyika kazi.

## Mwana-CCM Mkulima na Mfugaji

Watanzania wengi ni wakulima, wakulima ndio wengi zaidi. Mkulima kwa maana pana ni pamoja na mfugaji. Katika siku za nyuma, baadhi ya wanachama waliwahi kutiwa msukosuko kwa kuwa na mashamba makubwa au kufuga kuku 500. Lakini baadaye Chama kilijisahihisha kama inavyosema Programu ya Chama:

> Chama Cha Mapinduzi ni Chama kinachokua (haikudumaa). Kinakaa katika **nadharia** na **falsafa** yake, (ili kwenda na wakati).

Hii ndio ilivyokifanya Chama kijisahihishe kila kinapokosea.
Kwa hiyo kama siku moja tulimtia mwenzetu msukosuko kwa kuwa na shamba kubwa, mbuzi 18 au kuku 500, sasa Chama kimekua katika falsafa yake. Falsafa ya sasa inatia maanani hali halisi ya wakati wa sasa. Ndio maana kule Zanzibar tukaruhusu kiongozi awe na shamba lisilozidi hekta 20, hasa kama shamba hilo limo katika eneo la kijiji.

Kuhusu ufugaji, kuna baadhi ya wenzetu katika makabila ya Tanzania ambao kwao ni utamaduni wao kuwa na ng’ombe wengi. Mfano mzuri ni wenzetu wa makabila ya Wamasai, Wasukuma na Wagogo. Je, mwenye utamaduni wa kumiliki ng’ombe wengi akataliwe katika Chama kwa sababu ya kumiliki ng’ombe wengi? Tunasema hapana. Akiomba uanachama wa CCM akubaliwe. Chama Cha Mapinduzi hakimkatai tajiri aliyepata utajiri wake kwa njia ya halali na kulipa kodi ya Serikali analipa. Anayekataliwa na CCM ni yule aliyepata utajiri kwa wizi, kwa rushwa, dhuluma na kwa njia nyingine za haramu.

Huko Zanzibar tulifikiria labda tuweke kiwango maalum cha mifugo, kama vile iwe mwisho ng’ombe 200 peke yake. Lakini tulijiuliza kama ng’ombe mmoja akizaa na jumla kufikai 201, je huyo ndama amnyonge shingo?
Hiyo ndio hali halisi iliyotufanya tukubaliane kuwa mfugaji yeyote anaetaka kuwa mwanachama bila ya kujali idadi ya mifugo yake. Mwenye mshahara mkubwa, vile vile hata wa malaki, maadam ni mshahara wa kazi halali, naye pia aruhusiwe kuwa mwanachama wa CCM.

## Mafunzo ya Miezi Mitatu

Ili kukiimarisha zaidi Chama, tumewaruhusu wananchi kuwa wanachama wa CCM bila ya kuhudhuria yale mafunzo ya miezi mitatu.

## Biashara Ndogo Ndogo

Huko Unguja hatukuishia hapo. Tuliamua kuwa Mwanachama wa CCM wa kawaida naye pia aruhusiwe kuwa na biashara ndogo ndogo ili kumwongezea kipato. Biashara hizo, ambazo sharti zifanywe baada ya saa za kazi, ni pamoja na uvuvi, kuwa na gari ndogo au pick-up ya kukodisha kwa kuchukulia abiria au mizigo, kushona, kusindika matunda, mafuta na mashine ya kukoboa au kusaga unga.

Mwanachama mwenye mashine ya kusaga unga hanyonyi bali anatoa huduma kwa jirani zake kijijini. Chama na Serikali vimo mbioni kuhimiza na kutafuta teknolojia ya kumrahisishia kazi Mtanzania, hasa wanawake. Ni vyema kukaribisha teknolojia ya kuwasaidia wanawake waondokane na kufanya kazi ngumu ngumu zinazoweza kuwapotezea wakati na kuathiri afya zao, kama vile kutwanga au kusaga nafaka, kubeba mizigo ya kuni, maji na mtoto mgongoni. Si vyema kwa jamii yetu kuingia katika karne ya ishirini na moja katika hali hiyo. Ndio maana kule Zanzibar tuliamua kuruhusu biashara ndogo ndogo kuendeshwa na mwanachama wa CCM kwa manufaa yao na ya jamii.

Ndugu Wazee, haya kwa muhtasari ndio yaliyoamuliwa Zanzibar. Haya kamwe hayabomoi Azimio la Arusha, badala yake yanaliimarisha. Azimio la Arusha ni msingi wa siasa yatu ya Ujamaa na Kujitegemea. Ili tuweze kujitegemea lazima tuandae mbinu na mikakati ya kuzalisha mali, huduma na chakula. Hili ndio lengo la maamuzi ya Zanzibar.

Mshairi mmoja amesema:-

> Kutaraji uongofu bila kupitia njia zake ni kama kulitaka
> jahazi kutembea nchi kavu.
> Ndugu Wazee Ahsanteni sana. *(Makofi)*

# Sura ya Tano

# Miongozo Miwili ya Chama na Tabaka Lililopindua Ujamaa[3]

Issa Shivji

## Mwongozo wa TANU, 1971

Chama cha TANU kilichopigania uhuru wa Tanganyika chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ndicho kilichoasisi Azimio la Arusha mwaka wa 1967. Azimio liliweka mtazamo na sera za Ujamaa na Kujitegemea. Wakati ule nyaraka mbalimbali ziliandaliwa na kuandikwa ili kutoa miongozo katika kutekeleza Azimio la Arusha. Waraka muhimu mmojawapo ni **Mwongozo wa TANU wa 1971**. Mwongozo huo una umuhimu wa kipekee katika historia ya siasa za Tanzania. Mambo muhimu matatu yamezungumziwa katika Mwongozo huo. Mosi ni kutambua kwamba ubeberu unaendelea kunyanyasa na kunyonya Waafrika hata baada ya ukoloni kupitia sura yake mpya ya ukoloni-mamboleo. Kutokana na ukweli huo, "Vyama vya Siasa vya kimapinduzi katika nchi nyingi za Afrika zinazojitawala, kama vile TANU, bado ni ngali ni vyama vya ukombozi."

Pili ni umuhimu na ulazima wa kuunda jeshi la mgambo ambalo litalinda uhuru wa nchi dhidi ya maadui. Chimbuko la uamuzi huo linajulikana. Tanzania ilikuwa mstari wa mbele kusaidia ukombozi wa nchi za Afrika ambazo bado zilikuwa chini ya ukoloni. Wapigania uhuru ambao walikuwa wanasaidiwa na Tanzania moja kwa moja walikuwa wale wa Afrika ya Kusini, Namibia, wakati ule ikiitwa 'South West Afrika', na Msumbiji ambayo ilikuwa chini ya ukoloni katili wa Wareno.

[3] Makala haya yalichapishwa kwa mara ya kwanza katika jarida la *Chemchemi,* toleo na. 2, Oktoba 2009. Yamesahihishwa (revised) kwa ajili ya kitabu hiki.

Huko Afrika ya Magharibi, nchi mojawapo ambayo ilifanana sana na Tanzania katika sera zake na hasa katika kusaidia wapigania uhuru ilikuwa Guinea-Conakry chini ya uongozi wa Sekou Toure. Wapigania uhuru wa Guinea-Bissau na Cape Verde, ambazo zilikuwa nchi moja wakati huo, chini ya uongozi shupavu wa Amilcar Cabral, walisaidiwa na Sekou Toure. Kutokana na nafasi ya Guinea-Conakry katika vita vya ukombozi, majeshi ya Wareno yalivamia Guinea-Conakry. Hata hivyo hawakufanikiwa kwa sababu Guinea-Conakry iliweza kuwashinda, hasa kutokana na jinsi wanamgambo walivyopigana kwa ujasiri na ushupavu.

Isitoshe, karibu na nyumbani, Rais Obote wa Uganda alipinduliwa na jeshi lake chini ya Idi Amin Dada akisaidiwa na Uingereza na Israeli. Hii ilitokea baada ya Obote kutangaza kasiasa ka kajamaa na pia kuunga mkono nchi zilizokuwa mstari wa mbele katika ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika ambazo bado zilikuwa zinatawaliwa na wakoloni na makaburu.

Mambo haya yote mawili ni wazi yalikuwa tishio kwa Tanzania. Tanzania pia ilikuwa na wasiwasi wa kuvamiwa na jeshi la Wareno. Ndio maana chama na serikali waliamua kuwa na jeshi la wanamgambo. Jambo hili ni la kwanza linalozungumziwa katika Mwongozo wa Tanu, 1971. Pia, Tanzania ilikuwa haipendwi na mabeberu kutokana na siasa zake za kijamaa.

Pamoja na mambo haya, sifa moja ya Mwongozo ni uchambuzi wake wa radikali wa hali halisi ambao unaufanya Mwongozo nyaraka ya kimapinduzi kuliko zote zingine zilizoandikwa wakati wa enzi za Azimio la Arusha. Mfano mmoja tu unatosha kudhihirisha hili.

> Mapinduzi ni mabadiliko ya haraka katika jamii, mabadiliko ambayo yanawanyang’anya wachache madaraka ambayo walikuwa wakiyatumia kwa manufaa yao (na ya wanyonyaji wa nje), na kuyaweka madaraka hayo mikononi mwa wengi ili kuendeleza maslahi yao.

Katika hili, Chama chini ya uongozi wa Mwalimu, kwa mara ya kwanza, kimeweka wazi waadui wa Mapinduzi ya kijamaa, wakiwa vibaraka wa ndani wakiungwa mkono na wanyonyaji wa nje kwa maana ya mabepari wa kimataifa kutoka nchi za kibeberu.

***

Lakini zaidi ya yote jambo ambalo lilifanya Mwongozo uwe na historia ya kipekee ni ibara ya 15 ya Mwongozo. Ibara hii inasema:

> Lazima iwepo jitihada ya kujenga hali ya usawa kati ya viongozi na wanaowaongoza. Iwe ni mwiko kwa kiongozi wa Tanzania kuwa mwenye majivuno, ubadhirifu, dharau na uonevu. Kiongozi wa Tanzania awe ni mtu anayeheshimu watu, asiwe ni mpenda makuu, sio mnyapara, mkaripiaji na muamrishaji watu.

Ibara hii ikawa kauli mbiu na itikadi ya tabaka la wafanyakazi dhidi ya menejimenti yao viwandani. Takribani miaka minne kufuatia kutangazwa kwa Mwongozo, kuliibuka vuguvugu la wafanyakazi ambalo lilikuwa halijawahi kutokea katika historia ya nchi. Katika kipindi kifupi cha miaka mitatu tu (1971-1974), kulikuwa na migomo zaidi ya 30, ambayo ilihusisha wafanyakazi takriban 23,000 na siku za kazi zilizopotea ni takriban 64,000. Kwa kasi kubwa sana wafanyakazi walijifunza mikakati na mbinu za mapambano ya kitabaka. Walianza na migomo ya kawaida kwa maana ya kuweka chini zana za kazi. Kutokana na kulaumiwa kwamba wafanyakazi walikuwa hawajali maslahi ya taifa, wafanyakazi wakabadili mbinu zao katika awamu ya pili. Badala ya kugoma, wakaanza kuwafungia nje wanyapara na wamiliki wa viwanda wakati wakiendelea na uzalishaji.

Lakini kama unaweza kuzalisha bila menejimenti, kwa nini ukubali menejimenti? Kwa hivyo, mapambano yakakoma na wafanyakazi wakaanza kutwaa viwanda. Hapo ndipo, watawala wa kisiasa na kiuchumi wakashtuka. Viongozi wa chama na serikali wakaanza kuwashutumu wafanyakazi wazi

wazi kwa kusema kwamba ingawa chama kilikuwa na sera ya kutaifisha viwanda hii haikuwa na maana kwamba wafanyakazi wenyewe waanze mtindo huo. Utaifishaji lazima ufuate taratibu na ustaarabu!

Katika hotuba ya Mei Mosi (ya mwaka wa 1974) yenye kichwa cha habari *Ukigoma unamgomea nani?* Mwalimu aliwashutumu wafanyakazi, jambo ambalo mara moja lilivunja nguvu za wafanyakazi. Hotuba ya Mei Mosi ikawa mwongozo wa menejimenti au warasimu, nao walifurahia sana.

Kwa kweli, vuguvugu la wafanyakazi lilikuwa mapambano ya kitabaka dhidi ya tabaka la warasimu. Katika makala yangu ("*The Silent Class Struggle"* au Mapambano Baridi ya Kitabaka) iliyochapishwa na jarida la kimapinduzi la wanafunzi wanamapinduzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Cheche*, nilifanya uchambuzi na nikaliita tabaka hili jipya *mabepari wa kirasimu* (*bureaucratic bourgeoisie*). Baada ya mwaka mmoja nikaandika makala ya pili ambayo hatimaye ilichapishwa kama kitabu, kwa jina la *Class Struggles in Tanzania* (Mapambano ya Kitabaka Nchini Tanzania). Wakati ule watu wachache sana waliweza kukubaliana na uchambuzi wangu na viongozi walibeza kwamba Tanzania ni nchi ya wakulima na wafanyakazi na hakuna matabaka. Kwa kiasi fulani, kulikuwa na ukweli humu kwa sababu matabaka bado yalikuwa katika uchanga wake, yalikuwa hayajakomaa hasa kutokana na sera mbalimbali za Mwalimu za kuzuia viongozi na warasimu wasijilimbikizie mali (kwa mfano kwa kupitia katika Miiko ya Uongozi).

Kwa hivyo, nguvu ya tabaka la wafanyakazi ikavunjika na hatimaye kwa sheria ya 1975, wafanyakazi wakawekwa chini ya chama cha NUTA (National Union of Tanganyika Workers) ambacho kwa vyovyote vile kilikuwa chini ya himaya ya chama tawala.

Kwa upande mwingine, sera ya Chama juu ya vijiji vya ujamaa pia ikatekwa na wenye jazba na wapiga debe katika Chama. Mtazamo wa Ujamaa Vijijini ambao ulisisitiza kwamba vijiji vya ujamaa viwe chaguo la hiari la wakulima wenyewe ukageuzwa. Sera ukawa 'vijiji vya maendeleo' na

wanakijiji wakalazimshwa, mara nyingine chini ya ulinzi na mabavu ya FFU (Field Force Unit) kuhamia katika vijiji vya maendeleo. Jambo hili lilifanya wakulima waanze kupoteza imani na Chama. Kwa ufupi basi, matabaka ya wafanyakazi na wakulima wakafarakishwa na kutenganishwa na Chama, na kwa kiasi fulani Mwalimu mwenyewe. Kwa upande mwinigine, kuvunjika kwa nguvu za wavujajasho, uka safisha njia kwa warasimu na wamangimeza wa Chama na Serikali, kuendelea kujilimbikizia madaraka (na hata mali angalau kwa kificho) na kujijenga kama tabaka jipya la vibepari chini ya himaya ya ubeberu. Hawa ndio hatimaye wakaja kuainishwa kwa ufasaha kama wapingamapinduzi katika Mwongozo wa 1981.

## Mwongozo wa CCM, 1981

Kipindi cha mwisho cha Mwalimu Nyerere (1980-85) kilikuwa kigumu kuliko vyote katika utawala wake. Hali ya uchumi ilidorora kutokana na sababu mbalimbali za ndani na nje, pamoja na vita vya Uganda, ambavyo viliigharimu nchi sana; kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupanda kwa bei za petroli. Mnamo 1981, Chama tawala, wakati huo CCM, kilifanya tathmini ya miaka 14 ya Azimio la Arusha na kiliainisha hali halisi ya siasa, jamii na uchumi. Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa Chama kufanya uchambuzi wa kina bila ya kujali maslahi yake ya muda mfupi.

Kwa maoni yangu, hoja ambayo ni nzito katika uchambuzi huo ni kwamba chini ya mwavuli wa Azimio la Arusha na sekta ya umma, hususan mashirika ya "umma", lilijengeka tabaka jipya la mabepari. *Mwongozo* unasema:

> Kwani ukweli unaojitokeza wazi wazi ni kuwa baadhi ya matatizo yetu ya uchumi yanatokana na kutotekeleza kwa dhati siasa ya Ujamaa na Kujitegemea vijijini na katika sekta ya umma tuliyoianzisha. Zaidi ya hivyo, wakati mwingine katika miaka kumi na minne tangu Azimio la Arusha, Chama, Serikali, na vyombo vyake vilitumika kukuza sekta ya kibepari nchini katika viwanda, biashara, usafirishaji, ujenzi na kadhalika na ubepari huo uliopanuka katika kipindi hiki umeimarisha vitendo vya kuivuruga na

> kuidhoofisha sekta yetu ya Umaa (ib. 35, uk, 25).

Sehemu nyingine, *Mwongozo* unaendelea kueleza kwa ufasaha mkubwa kwamba:

> Leo ubepari una vishawishi vingi zaidi nchini kuliko ulivyokuwa kabla ya Azimio la Arusha kwa sababu pamoja na kwamba sasa tuna sekta kubwa ya umma lakini kutokana na udhaifu wa kutopambana nao, ubepari umefaulu kujipanua na kujipenyeza hata ndani ya sekta yenyewe ya umma. Na ndio maana ubepari sasa unathubutu kujitokeza hadharani kuukashifu Ujamaa, kubabaisha baadhi ya viongozi na kututaka tubadilishe siasa yetu (ib. 52, uk.39-40).

Kwa hakika matamko haya yalikuwa ni kukiri wazi wazi kwamba sera za Ujamaa zilikuwa zimehujumiwa na viongozi wenyewe waliopewa jukumu la kuongoza ujenzi wa Ujamaa kutokana na maslahi yao ya kitabaka ya kibepari.

Hapa tunashuhudia kwa mara ya kwanza, Chama kikikiri kwamba kuna mapambano au harakati za kitabaka dhana ambayo kila mara Chama, na hasa Mwalimu mwenyewe, alikuwa anaikanusha. Kinadharia na kiitikadi Mwalimu hakukubaliana kabisa na dhana ya mapambano ya kitabaka. Hata hivyo ibara ya 50 ya *Mwongozo* inaenda mbali zaidi kwa kueleza kwamba:

> Kuielewa vema jamii ya Tanzania ya leo kunataka uchambuzi wa hali ya juu pia. Uchambuzi huu ukiwezeshe Chama kuielewa migongano ya maslahi ya tabaka ambayo imejitokeza nchini. Migongano hii ina mizizi katika mgongano wa msingi kati ya Ujamaa na ubepari, kati ya maslahi ya wakulima na wafanyakazi kwa upande mmoja, na ya ubinafsi, ubwanyenye na ubepari ambao umekuwa ukijengeka tangu Azimio la Arusha kwa upande mwingine. (uk.37-38).

Uchambuzi huo ni wazi na umefanywa kwa ufasaha na kisayansi. Swali muhimu kwa wasomi, wanazuoni na wakereketwa wa Usoshalisti ni: Je, Chama kilifanikiwa katika mapambano haya na kurudisha nchi kwenye Ujamaa? Au tabaka hili liliojengeka lilishinda mapambano na ndilo injini inayosukuma gurudumu la mageuzi ya kisiasa na kiuchumi kuelekea kwenye uliberali mamboleo, ambao ni mfumo wa kibepari? Je, tabaka hilo la mabepari warasimu ndilo hasa chimbuko la mfumo huo wa ubepari uchwara, ukiungwa mkono na ubeberu, na ambao ndio unatutawala leo? Je, si kweli kwamba, katika awamu hasa ya tatu tabaka hili la mabepari warasimu ndilo lililokuwa mstari wa mbele kutetea ubepari wakimnukuu kwa furaha Deng Tsio-Ping, kiongozi wa China, aliyepindua ujamaa nchini China?

Katika mahojiano yake na mwandishi wa habari Jonathan Power wa jarida la *Prospect* (na. 112, Julai 2005), Rais mstaafu Benjamin Mkapa alikiri kwamba yeye alikuwa anamheshimu Deng Tsio-Ping. Alipoulizwa na Jonathan Power kwamba je, Nyerere akifufuka angesema je, Mkapa akamjibu: 'Angesema kwamba mimi nimegawia mengi yaliyokuwa katika sekta ya umma. Na angefadhaishwa na ukweli kwamba mimi nimefanikiwa kujenga tabaka la mabepari matajiri.'

Sina hakika kama Rais Mkapa alifanikiwa kujenga tabaka la mabepari matajiri au alijenga tabaka la vibepari uchwara tu. Ni suala la kufanyiwa utafiti. Haikuwa nia yangu kuangalia suala hili kwa undani bali ni kudokeza tu kwamba kama tunataka kuelewa vyema na kisayansi hali halisi ya nchi na jamii yetu ya leo hatuna budi kufanya uchambuzi wa kitabaka katika mfumo wa ubepari uchwara chini ya utawala wa kibeberu, hususan, tabaka lililoongoza mageuzi. Na hoja yangu ni kwamba Mwongozo wa CCM wa 1981 unatuweka mahali pazuri pa kuanzia. Kazi kwetu!

Ni jukumu la wasomi na wanazuoni kuchambua jamii yao, kuionyesha jamii sura yake halisi na kuainisha mielekeo ya maendeleo na mielekeo ya wapinga mendeleo. Kama Mwongozo wa 1981 unavyosema : mapinduzi sio

lelemama. Mapinduzi yanahitaji wakereketwa wa kijamii ambao msimamo wao kwa upande wa wavujajasho hautetereki:

> Ujenzi wa ujamaa si lelemama bali ni mapambano, mapambano ya kudumu dhidi ya ubepari na unyonyaji, dhidi ya wapinga maendeleo na wababaishaji wa kisiasa, dhidi ya wahujumu uchumi, majambazi, wezi, wazururaji na wazembe. Msimamo sahihi wa mapambano unaotokana na nadharia sahihi ya ujamaa ungelituepusha na maamuzi na vitendo ambavyo vimerahisisha kuoteshwa kwa mizizi ya ubepari, kinyume cha msimamo wa mapambano dhidi ya ubepari. Leo ubepari, una vishawishi vingi zaidi nchini kuliko ulivyokuwa kabla ya Azimio la Arusha kwa sababu pamoja na kwamba sasa tuna sekta kubwa ya umma lakini kutokana na udhaifu wa kutopambana nao, ubepari umefaulu kujipanua na kujipenyeza hata ndani ya sekta yenyewe ya Umma. Na ndiyo maana ubepari sasa unathubutu kujitokeza hadharani kuukashifu ujamaa, kubabaisha baadhi ya viongozi na kututaka tubadilishe siasa yetu. (ibara ya 52)

Ukweli uliojitokeza tangu uchambuzi huo wa Mwongozo wa 1981 ni kwamba, ubepari uliosimamiwa na vibepari uchwara wa ndani na nchi za kibeberu (ambao siku hizi wanaitwa eti washirika wetu wa maendeleo) umeshinda katika mapambano. Chini ya visingizio mbalimbali, pamoja na fikra hafifu ya "kwenda na wakati", Azimio lilipinduliwa na hadi sasa uliberali mambo-leo unaendelea kutamalaki.

*Marejeo*

Mapolu, Henry (ed.) (1976), *Workers and Management* (Dar es Salaam : Tanzania Publishing House)

Mapolu, Henry na Issa Shivji (1984), *Vuguvugu la Wafanyakazi Nchini Tanzania* (Kampala : Urban Rural Mission)

Mihyo, P. (1975), 'The Struggle for Workers Control in Tanzania', *Review of African Political Economy,* No.4.

Shivji, Issa G. (1976), *Class Struggles in Tanzania* (Dar es Salaam, London & New York : Tanzania Publishing House, Heinemaan and Monthly Review).

Shivji, Issa G., (1970), *Tanzania : The Silent Class Struggle* (Cheche 1970) na kuchapishwa tena katika Issa G. Shivji (ed.) na wengine : *The Silent Class Struggle* (1972, Tanzania Publishing House.

**Maelezo ya Sura ya Kwanza**

1 C. L. R. James, 1982, Nkrumah and the Ghana Revolution, London: Allison & Busby.

2 Julius K. Nyerere, 1968, 'Azimio la Arusha' katika Ujamaa, Dar es Salaam: Oxford University Press, uk. 13-35, uk. wa 17. Angalia Sura ya Pili.

3 Mwalimu Nyerere alirejea katika historia hiyo alipokuwa anawaaga Wazee wa Dar es Salaam wakati anang'atuka.

4 Imenukuliwa katika Cranford Pratt, 1976, The critical phase in Tanzania, 1948-1968: Nyerere and the Emergence of a Socialist Stratgey, Cambridge: Cambridge University Press, uk. 233.

5 Pratt, 1976, Critical Phase, uk. 234.

6 TANU, 1967, Hotuba ya Baba wa Taifa (Julius Nyerere) katika Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa, 26 January – 28 January, 1967, Makavazi ya CCM, Dodoma, uk. 7.

7 Nyerere, 1968, Ujamaa, uk. 16.

8 Nyerere, 1968, Ujamaa, uk. 16.

9 Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, 1967, Azimio la Arusha: Majibu kwa Maswali, Dar es Salaam: Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, uk. 2.

10 Jamhuri wa Muungano, 1967, Azimio: Majibu kwa Maswali, uk. 3.

11 Jamhuri wa Muungano, 1967, Azimio: Majibu kwa Maswali, uk. 3.